# MAUDHUI YA SIASA NA ATHARI ZAKE KATIKA JAMII: MIFANO KUTOKA *DIWANI YA KAZA MACHO*

**JOMO VIOS ONDORO**

**C50/89887/2016**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2021**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

**Jomo Vios Ondoro**

**C50/89887/2016**

**Sahihi** ______________ **Tarehe** 14-11-2021

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**Sahihi** ______________ **Tarehe** 14/11/2021

**PROF. RAYYA TIMAMMY**

**(Msimamizi)**

**Sahihi** ______________ **Tarehe** 14/11/21

**PROF. KINENE WA MUTISO**

**(Msimamizi)**

## TABARUKU

Tabaruku yangu iwaendee wazazi wangu wapendwa bwana Jomo Ongaki, Margret Kwamboka pamoja na nyanyangu Nyaboke na ndugu zangu Fred, Kerubo, Rose na binamu yangu Ouko kwa maombi yenu ya kipekee wakati wa masomo yangu ya uzamili.

## SHUKRANI

Namshukuru Maulana aliyenijalia uzima, siha njema na mawazo na kuniwezesha kukamilisha utafiti huu.

Shukrani za dhati pia ziwaendee wasimamizi wangu wa utafiti huu Prof. Rayya Timammy na Prof. Kinene wa Mutiso kwa kunishauri, kunipa motisha na mwongozo wa kitaaluma. Kwa hakika ushauri wenu ulinifaa pakubwa. Mungu azidi kuwaongezea busara na maarifa zaidi.

Shukrani za kipekee pia ni kwa wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi. Hawa ni Prof. Rayya Timammy, Prof. Kinene wa Mutiso, Prof. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. K.W. Wamitila, Dkt. Prisca Jerono, Dakt. Zaja Omboga, Dakt. Jefwa Mweri, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Mary Ndung'u na Mwalimu Sanja Leo. Asante sana kwa mijadala yenu iliyonifaidi ndani na nje ya Chuo.

Nashukuru familia yangu iliyoniombea na kunipa moyo hadi nikakamilisha masomo yangu. Shukrani za kipekee pia kwa mke wangu, Elizabeth Kerubo kwa msaada wa kifedha licha ya majukumu mengi ya kibinafsi yaliyomkabili. Kwa Watoto wangu Franklin, Neema na Lewis kwa kuvumilia upweke nilipokuwa chuoni. Mwenyezi Mungu awabariki.

Nawatambua wasomi wenzangu: Nancy Chepchirchir, Dickens, Nicodemus, Njane, Gacheru, Jacinta, Ogello, Lucy, Ruth, Rehema miongoni mwa wengine kwa mchango wenu darasani uliotokana na mijadala.

Marafiki zangu wapendwa kazini, Judith Kobia, Omwario, Patrick, Rakula, Mwangi, Amkah na Mullah. Hawa walinihimiza na kunishauri kwa kipindi hiki cha masomo yangu. Sitaweza kutaja kila mmoja aliyenifaa kwa njia moja au nyingine. Kwenu nyote nasema asante sana na Mola awabariki.

**Orodha ya Vifupisho**

| | |
|---|---|
| K.V. | Kama vile |
| K.M. | Kwa Mfano |
| N.K. | Na Kadhalika |
| Uk. | Ukurasa |
| KANU | Kenya African National Union |
| ODPP | Office of Director of Public Prosecutions |

**Ikisiri**

Kwenye tasnifu hii, tumehakiki maudhui ya siasa na athari zake katika jamii. Diwani ya *Kaza Macho* imerejelewa. Utafiti wetu ulilenga kutekeleza madhumuni matatu yafuatayo: Kuchanganua namna maudhui ya kisiasa yanavyojitokeza katika diwani hiyo. Pili, kubainisha athari za siasa kwa jamii. Na mwisho, kuchanganua mbinu za kisanaa ambazo zilitumiwa na K.W. Wamitila kuendeleza maudhui ya siasa katika diwani hiyo. Nadharia ya uyakinifu wa kijamii imetumika hapa. Mihimili ya nadharia hii ifuatayo ilitufaa sana: Wahusika wameonyeshwa kwa njia ya kiuyakinifu, nadharia hii imesawiri matukio ya kihistoria na wahusika wake kutekeleza matendo yao kitabaka. Utafiti wetu ulikuwa wa maktabani. Tulisoma diwani *Kaza Macho* kwa kina na kunukuu katika shajara sehemu muhimu ambazo zinalenga malengo yetu. Tulisoma magezeti mbalimbali, tasnifu za wasomi tofauti tofauti, vitabu vya ziada pamoja na kupekua mtandao ili kupata data. Tulichanganua data hiyo kwa kuzingatia madhumni ya utafiti wetu. Uchanganuzi wa data ulifanyika kwa kutumia njia ya uchambuzi wa kimaelezo na ufafanuzi.

## YALIYOMO


| | |
|---|---|
| **UNGAMO** | ii |
| **TABARUKU** | iii |
| **SHUKRANI** | iv |
| **Orodha ya Vifupisho** | v |
| **Ikisiri** | vi |
| **SURA YA KWANZA** | 1 |
| **1.0 Utangulizi** | 1 |
| **1.1. Tatizo la Utafiti** | 2 |
| **1.2 Madhumuni ya Utafiti** | 3 |
| **1.3 Maswali ya Utafiti** | 3 |
| **1.4 Sababu za Kuchagua Mada** | 4 |
| **1.5 Upeo na Mipaka** | 4 |
| **1.6 Msingi wa Kinadharia** | 5 |
| **1.6.1 Mihimili ya Nadharia** | 7 |
| **1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada** | 7 |
| **1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia.** | 12 |
| **1.8 Mbinu za Utafiti** | 13 |
| **1.8.1 Njia za kuteua Sampuli** | 13 |
| **1.8.2 Njia za Kukusanya Data** | 13 |
| **1.8.3 Uchanganuzi wa Data** | 14 |
| **1.8.4 Kuwasilisha Data** | 14 |
| **1.9 Hitimisho** | 14 |
| **SURA YA PILI:** | 15 |
| **UCHANGANUZI WA MAUDHUI YA SIASA** | 15 |
| **2.0 Utangulizi** | 15 |
| **2.1 Maudhui ya Siasa** | 15 |
| **2.1.1 Uongozi wa Kiimla.** | 16 |

**2.1.2 Ukiukaji wa Haki za Kibinadamu** **19**

**2.1.2.1 Wizi wa Haki ya Mpiga Kura** **19**

**2.1.2.2 Haki ya Kupata Lishe Bora.** **22**

**2.1.2.3 Haki ya Kupata Makazi Bora.** **23**

**2.1.3 Usaliti** **23**

**2.1.4 Ufisadi** **25**

**2.1.5 Ukiukaji wa Sheria** **27**

**2.1.6 Ukoloni** **29**

**2.1.7 Ukoloni Mamboleo** **30**

**2.2 Hitimisho** **31**

**SURA YA TATU:** **33**

**ATHARI ZA SIASA KWA JAMII** **33**

**3.0 Utangulizi** **33**

**3.1 Umaskini** **33**

**3.2 Tamaa na Unyanyasaji** **38**

**3.3 Utabaka** **40**

**3.4 Vita na Tanzia** **42**

**3.5 Viongozi Kung'atuliwa Mamlakani.** **44**

**3.6 Utamaushi** **45**

**3.7 Hitimisho** **45**

**SURA YA NNE:** **46**

**MBINU ZA KISANAA** **46**

**4.0 Utangulizi** **46**

**4.1 Tamathali za Usemi.** **46**

**4.1.1 Jazanda** **46**

**4.1.2 Tashbihi** **47**

**4.1.3 Tabaini** **48**

**4.1.4 Tanakali za Sauti** **49**

**4..1.5 Maswali ya Balagha** **49**

**4.1.6 Urudiaji.** **50**

**4.1.6.1 Urudiaji wa Neno** **51**

**4.1.6.2 Urudiaji wa Sauti (konsonanti na irabu)** **52**

**4.1.6.3 Urudiaji wa Mistari** 52
**4.1.6.4 Epifora** 52
**4.1.6.5 Anadiplomasia** 52
**4.1.6.6 Anafora** 53
**4.1.7 Usambamba** 53
**4.1.7.1 Usambamba wa Kitanakuzi** 53
**4.1.7.2 Usambamba wa Kifahiwa** 53
**4.1.8 Uhuishi** 54
**4.1.9 Chuku** 54
**4.1.10 Kinaya** 55
**4.1.11 Sitiari/Istiari** 55
**4.2.0 Mbinu Nyingine za Lugha** 56
**4.2.1 Methali** 56
**4.2.2 Nahau** 57
**4.2.3 Taswira** 57
**4.2.4 Kisengere Nyuma** 58
**4.2.5 Mdokezo** 59
**4.18 Hitimisho** 60
**SURA YA TANO** 61
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** 61
**5.0 Utangulizi** 61
**5.1 Muhtasari** 61
**5.2 Hitimisho** 63
**5.3 Mapendekezo** 63
**Marejeleo** 65

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Utafiti wetu unahusu kuhakiki maudhui ya siasa na athari zake katika diwani ya *Kaza Macho.* Diwani ya *Kaza Macho* imeandikwa na Kyallo Wadi Wamitila na kuchapishwa mwaka wa 2014. Amata na King'ei (2001), wamefafanua maudhui kama jumla ya mambo, mafundisho, mawazo ama ujumbe ambao unawasilishwa na mshairi kwa hadhira yake. Isitoshe, wanasema kwamba maudhui katika shairi hutokana na jamii ya mwandishi na wala si kutokana na ombwe tupu. Maoni haya yanashabihiana na ya Wamitila (2003) kwamba msanii hupata kariha ya kutunga mashairi yake kutokana na masuala ambayo yanamkera au kumgusa katika jamii yao. Tunaafikiana nao kuwa maudhui ni maswala yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi na hujengwa kwenye misingi ya dhamira.

Siasa imefafanuliwa kama njia ya kufanya maamuzi katika mji, taifa au dunia. Adero (2005:11) anasema kwamba siasa ni dhana ambayo inatumika kuelezea mfumo wa kuendesha masuala yanayokumba jamii katika taifa fulani. Tunakubaliana na maelezo hayo kwamba siasa huwa njia inayotumika kuitawala na vile vile kuiongoza jamii au nchi. Siasa huamua eneo au mahali ambapo pataendeshewa miradi mbalimbali. Kwa mfano, huamua mahali ambapo barabara itajengwa na inajengwa, ni sehemu gani zahanati itajengwa na inajengwa na ni eneo gani shule itajengwa. Endapo basi pataishia kutotekelezwa kwa miradi hiyo, sababu huwa ni kutokana na siasa (Bibiana, 2014).

Hivyo, katika utafiti wetu, tunanuia kuhakiki maudhui ya kisiasa na athari zake katika jamii. Suala la siasa haliwezi kutenganishwa na maisha ya binadamu katika jamii. Uongozi wa nchi hutegemea siasa za viongozi wa nchi hiyo. Siasa mbaya huharibu na kuporomosha uchumi wa nchi ilhali siasa nzuri hufufua na kuendeleza uchumi wa taifa mbali na kukomboa jamii dhidi ya kukumbwa na janga la umasikini, magonjwa, njaa, ujinga n.k. Diwani ya *Kaza Macho* imeangazia suala hili.

Katika nchi zinazoendelea hasa za Afrika, kumekuwa na siasa mbaya. Wanasiasa huonekana kupora mali ya umma na kushiriki katika ufisadi. Siasa hizo zimekuwa za ulaghai na utapeli. Wapiga kura husalitiwa kutokana na ahadi zisizotekelezwa. Kibwana (1996) anaeleza jinsi ambavyo wanasiasa nchini Kenya katika miaka ya tisini walibadilika kutoka kuwa viongozi

wazalendo na badala yake kuwa viongozi fisadi. Anabainisha haya kwa kutoa mfano wa jinsi ambavyo chama cha KANU (Kenya African National Union) kilitumia hela nyingi kuwanunua na kuwarai wapinzani kujiunga nacho ndipo waweze kuua na kumaliza upinzani.

Hatimaye mfumo wa utawala wa chama kimoja katika mataifa mengi ya Afrika ikiwemo Kenya, ulisambaratika na kupisha mfumo wa vyama vingi. Hii ilionekana kama hatua kubwa ya kisiasa ambayo ilidhaniwa itatupilia mbali uongozi wa kidikteta wa chama kimoja. Kinyume na ilivyotarajiwa na wananchi, viongozi hao walivitumia vyama hivyo kwa maslahi yao ya kibinafsi. Wanasiasa hao hushindana na kuzua mizozo au migogoro kutokana na kuchochea hisia za wafuasi wao. Matokeo yake huwa kugawanya watu katika misingi ya vyama vya kisiasa na kikabila. Vita huzuka hatimaye haswa wakati wa uchaguzi na kuwaacha wananchi wakiwa katika hali ya ulitima.

Tunaafikiana na mawazo ya Adero (2005:21) kuwa siasa inahusu mitafaruku katika jamii. Njia ambazo zitatumiwa na wanasiasa hao kuitatua mitafaruku hiyo zitaathiri maisha ya kila mja. Utafiti huu utachunguza diwani ya Wamitila (2014) *Kaza Macho* kwa undani na kupata taswira kamili za athari zinazotokana na siasa. Mashairi katika diwani ya *Kaza Macho* yanaangazia mawanda yote ya maisha ya watu kwa jumla hasa katika bara la Afrika. Tutaangazia mashairi ambayo yanashughulikia maswala ya kisiasa.

### 1.1. Tatizo la Utafiti

Suala la siasa linaonekana kuibua mjadala mkali katika jamii kutokana na kuwepo kwa mwingiliano wake na shughuli ambazo ni za kijamii. Mathalani, katika taifa letu la Kenya, walioko serikalini na wafuasi wao huonekana kupendelewa ilhali wanaopinga serikali huonewa na wakati mwingine kunyimwa nafasi ya kutolea maoni yao. Wananchi waliwakabidhi mamlaka wanasiasa kwa kuwapigia kura bila kupiga darubini maadili yao. Baadhi ya wanasiasa waliokuwa na tabia za kutiliwa shaka, walitukuzwa na wananchi. Viongozi hao ikiwemo magavana, wabunge, maseneta, wawakilishi wa akina mama pamoja na vibaraka wao walipinga vikali maoni kinzani dhidi yao.

Wananchi wametaabika sana kwa kukosa huduma za kimsingi na kushuhudia visa vya ubadhirifu na unyakuzi wa mali ya umma kutoka kwa hao viongozi. Kila msimu wa uchaguzi, kumeshuhudiwa vifo, machafuko na uharibifu wa mali. Uwepo wa masuala haya katika jamii ni

dhihirisho tosha kwamba wananchi wana upungufu wa elimu inayoangazia maisha yao hasa kisiasa.

Fasihi ikilinganishwa na kioo katika jamii huwa na jukumu la kuangazia uozo huo.
Siasa mbaya ni tatizo ambalo limelemaza maendeleo katika mataifa ya Afrika Mashariki Kenya ikiwa mojawapo. Hii ni kwa sababu ya kuwa na viongozi wanaojali maslahi yao tu. Viongozi hao wamejawa na ubinafsi na tamaa, hali ambayo imewatamausha wananchi.
Sampuli hii ya wanasiasa hutawala mataifa yao kiimla kwa kutumia mbinu fiche kwa lengo la kutimiza maslahi yao. Kwa maoni yetu, tatizo hili halijatafitiwa kwa mapana hasa na wasomi wa Kiswahili. Kwa hivyo, kuna umuhimu wa kuhakiki ni vipi maudhui ya kisiasa yalivyojitokeza katika diwani *Kaza Macho* na athari zake. Hili ndilo pengo tulilonuia kuliziba.

Pia, tulitathmini jinsi ambavyo mwandishi wa diwani hiyo, K.W. Wamitila (2014) amechangia katika kuizindua na kuielekeza jamii ili kukoma kuendeleza siasa mbaya. Kupitia usomaji wa kazi hii, wasomaji watapata mafunzo ambayo yatawafanya kuleta mabadiliko katika jamii.
Kutokuwepo kwa marejeleo muhimu kuhusu diwani hiyo, kunaashiria pengo katika utafiti wa mashairi katika fasihi. Tunatumai kuwa utafiti huu utakuwa msingi muhimu wa marejeleo katika fasihi.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti wetu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

i. Kuchanganua namna suala la kisiasa linavyojitokeza katika *Kaza Macho*.
ii. Kubainisha athari za siasa zinazojitokeza katika diwani ya *Kaza Macho*.
iii. Kuchanganua mbinu za kisanaa zilizotumiwa kuendeleza maudhui ya kisiasa katika diwani *Kaza Macho*.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Maswali yafuatayo yalinuiwa kujibiwa kwa minajili ya kuwezesha kukamilika kwa malengo ya utafiti.

i. Ni masuala gani ya kisiasa yanayojitokeza katika diwani ya *Kaza Macho*?

ii. Maudhui ya siasa yanaibua athari zipi kwa jamii katika diwani ya *Kaza Macho*?
iii. Mtunzi, Wamitila (2014), ametumia mbinu gani za kisanaa kuibua masuala ya kisiasa katika diwani?

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Suala la siasa ni suala muhimu katika maisha ya wanajamii na limeangaziwa sana hasa katika diwani ya *Kaza Macho* ambayo imeandikwa na Kyallo Wadi Wamitila. Suala hili huibua hisia mseto katika jamii kama tulivyoeleza katika utangulizi. Kutokana na kuwepo kwa juhudi au harakati za kujenga jamii mpya, utafiti huu utakuwa nyenzo bora ya kutolea mchango wetu dhidi ya kujihusisha na siasa mbaya.

Tumetafiti mada hii kutokana na sababu kwamba siasa katika nchi zinazoendelea zimekuwa za ulaghai na utapeli, ufisadi kukita mizizi pamoja na uporaji wa mali ya umma. Wananchi husalitiwa mara kwa mara kwa kutotekelezwa miradi mbalimbali na kuishia kusalia maskini.

Mbali na kutoa mchango wetu katika uhakiki wa fasihi, mada hii pia tumeichagua ili kuwawekea watafiti wengine wa baadaye msingi ambao watatumia kutafitia mada zingine katika diwani hii ya *Kaza Macho*. Kutokana na upekuzi wetu, tumegundua kwamba kitabu hiki cha *Kaza Macho* hakijatafitiwa. Kwa hivyo, pamekuwa na pengo la kiusomi ambalo limetutia changamoto ya kutaka kuliziba na hivyo kuchangia katika ukuaji wa fasihi.

## 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulinuia kuhakiki maudhui ya kisiasa na athari zake katika jamii kwa kurejelea diwani, *Kaza Macho* iliyochapishwa na Wamitila (2014). Diwani hii ina jumla ya mashairi sabini na tatu. Katika uhakiki huu, tumeangazia kwa kusoma kwa kina mashairi arubaini na tano ambayo ni mafupi mafupi yafuatayo: Uonacho Sicho (uk.1), Msalaba (uk.2), Mfumo wa Soko Huria (uk.3), Kivuli (uk.5), Kwa Nini? (uk.6), Meli, Nini Kiliipata? (uk.8), Mwanasiasa (uk.11), Mlevi wa Historia (uk.12), Tazama (uk.14), Uhuru (uk.15), Kibinimethali (uk.16), Kaza Macho (uk.17), Ulifanya nini (uk.18), Mgonjwa (uk.19), Kadhia ya Jana (uk.21), Jikanye (uk.23), Mwanga (uk.24), Jana na Leo (uk.26), Ushamwona? (uk.29), Zinduka (uk.31), Kiokote (uk.34), Lini? (uk.36), Sera (uk.38), Nyota ya Huzuni (uk.40), Pendo (uk.41), Jogoo (uk.42), Anguko la Jibwa (uk.43), Ndege wako Mashakani (uk.45), Siku ile Kanisani (uk.48), Mkuki kwa Nguruwe (uk.51), Chini ya Mgunga (uk.53), Nungubandia (uk.55), Ijumaa (uk.57), Kibuyu (uk.58), Adha

yetu (uk.60), Ina nini? (uk.71), Kichekesho cha Historia (uk.74), Kipofu na Kichaa (uk.78), Kikao cha Wanasiasa (uk.89), Kumekucha (uk.90), Mpanda Ngazi na Washika Ngazi (uk.95), Utenzi wa Ndovu na Mja (uk. 105), Niko Hapa (uk.113), Jumamosi (uk.123) na Uliambiwa (uk.126). Tumechunguza mashairi hayo kulingana na maudhui ya kisiasa na siyo mengine isipokuwa pengine pale yatakuwa yamefungamana na siasa.

Tumeiteua diwani hii kimakusudi na vile vile kutokana na sababu kuwa maudhui ya kisiasa yamepewa nafasi kubwa na mtunzi wake. Hii ina maana kuwa tutapata data za kutosheleza utafiti wetu. Wahusika katika diwani hii wameathirika na siasa na wakati mwingine kuhisi kwamba haki zao zimekiukwa.

**1.6 Msingi wa Kinadharia**

Tumetumia nadharia ya uyakinifu wa kijamii kutuongoza kuchanganua maudhui ya siasa na athari zake katika diwani *Kaza Macho*. Nadharia hii inaweka msisitizo kwenye msingi wa hali za kiuyakinifu za maisha. Kulingana na Owallah (2013), nadharia hii huangazia uhalisia wa kijamii na mikinzano inayotokea katika jamii ambayo inaleta tofauti za kitabaka. Hivyo basi, nadharia hii hulenga kuhamasisha na kuzindua masikini ambao wanakandamizwa ndipo waweze kufahamu na kuanza kupigania haki zao.

Mwasisi wa nadharia hii ni Stalin na aliiasisi mwaka wa 1917. Stalin aliweza kuathirika na Umaksi ambapo alipata nia ya kutaka kubadilisha jamii au nchi yake ya Urusi. Umaksi uliasisiwa na Karl Marx baina ya mwaka wa 1818-1863 na ulilenga kuangazia maswala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni. Pia, unajadili uhusiano na mapambano ya kitabaka kati ya mamwinyi na makabwela. Kulingana na umaksi, mfumo wa uzalishaji mali katika hali halisi ya maisha ndio unaoelekeza hali za kisiasa, kijamii, kitamaduni na kiuchumi (Kimeu, 2016:4).

Hivyo basi, endapo mabadiliko ya kiuchumi yatatokea, muundo mzima wa taasisi ya kijamii hubadilika. Stalin aliweza kutumia mwongozo huu wa nadharia hii ya umaksi kuangazia uyakinifu katika maisha. Alifanya hivyo aliposawazisha watu katika nchi ya Urusi kwa kutumia mapinduzi yake dhidi ya watu wachache waliokuwa wanatawala nyanja za kisiasa, kisosholojia na kiuchumi. Nadharia ya Uyakinifu wa Kijamii hupigania kuichora jamii katika uhalisia pamoja na ukamilifu wake na hivyo kuonyesha mabadiliko na hatua zake. Hivyo basi, katika kuchanganua athari za siasa katika diwani ya *Kaza Macho*, inatubidi tuimulike jamii kwa ukamilifu wake.

Stalin aliweza kuhamasisha jamii yake kwa lengo la kulizindua tabaka la chini ambalo lilikuwa linanyanyaswa ili liweze kufahamu haki zao na kuzitetea dhidi ya tabaka lile la juu la kibepari. Wataalamu mbalimbali wameweza kutoa mchango wao kuhusu nadharia hii ya uyakinifu wa kijamii baada ya kuasisiwa kwake. Wataalamu hawa ni pamoja na Gorky (1973), Brecht na Patrick (1973), Senkoro (1987), Wamitila (2003) na Muriithi (2013).

Gorky (1973), anafafanua nadharia hii na kusema kuwa ni mwonoulimwengu wa binadamu ambao wanabadilisha na kusababisha ujenzi mpya wa ulimwengu. Anaendelea kusema kwamba wajibu wa jamii ni kuleta mabadiliko katika maisha ya waja na vipengele vyote vinavyomhusu kama vile siasa na uchumi. Diwani ya *Kaza Macho* kama kazi ya fasihi inatekeleza jukumu hili hasa kupitia mashairi ya Mwanasiasa (uk.11), Mlevi wa Historia (uk.12), Mpanda Ngazi na Washika Ngazi (uk.95) n.k.

Brecht na Patrick (1973) pia, wanatoa maelezo kwa kusema kuwa Uyakinifu wa Kijamii ni sanaa ambayo inapambana na fikra za uongo zinazohusu uhalisia wa kijamii pamoja na hisia zinazoleta mtafaruku katika maslahi ya watu. Maelezo haya yanaonyesha mvutano wa kitabaka ulioko katika jamii ambapo tabaka la chini huzinduliwa ili kupigania haki zao kutoka kwa tabaka la juu. Katika shairi la Mpanda Ngazi na Washika Ngazi *(*uk.95*)* katika diwani ya *Kaza Macho*, Washika Ngazi ni kiwakilishi cha wapiga kura ambao wameudhika na kukerwa na tabia za wanasiasa ambao wanawakilishwa na Mpanda Ngazi. Wanasiasa hutumia uongo kuomba kura na baada ya kuchaguliwa, wao huwasaliti waliowapigia kura. Kulingana na Brecht na Patrick (1973), 'usawa kwa wote' unaweza kupatikana endapo tu kila mja atazinduka na kupata ukweli wa mambo halisi.

Naye Wamitila (2003), akitoa mchango wake kuhusu nadharia hii anasema kwamba nadharia hii inasisitiza uhalisia kuwa muhimu katika kutilia mkazo njia za kimaendeleo haswa kihistoria. Akichangia kuhusu nadharia hii, Senkoro (1987) anasema kuwa nadharia hii ni kitengo cha juu cha uchambuzi wa uhalisia. Anaendelea kusema kwamba binadamu amekuwa nguzo kuu inayosababisha matabaka katika jamii. Anaongezea kusema kwamba masuala yote ambayo yanamhusu binadamu yasifichwe na yaweze kuwekwa wazi ili mabadiliko yafanyike. Mawazo ya wataalam hawa wote yatatufaa katika kuhakiki maudhui ya kisiasa kama suala ambalo linaathiri jamii kwa ujumla.

Muriithi (2013) akimnukuu Lucaks (1963), anaieleza nadharia hii ya Uyakinifu wa Kijamii kwamba ina uwezo wa kuisawiri jamii katika ukamilifu wake na hivyo kuonyesha hatua zake za kimabadiliko. Kulingana na Lucaks (1963), nadharia hii ya Uyakinifu wa Kijamii husawiri hali halisi ya kijamii pamoja na hatua zilizochukuliwa katika mabadiliko yake ya kisosholojia

### 1.6.1 Mihimili ya Nadharia

Nadharia hii ina mihimili ifuatayo: Mosi, wahusika wake huonyeshwa kwa njia ya kiuyakinifu. Wahusika hao humithilishwa na binadamu wa kawaida ambao wanaishi katika ulimwengu huu tunaoujua. Mhimili huu utatusaidia sana kuchanganua maudhui haya ya kisiasa kwa kurejelea diwani. Kwa mfano, katika shairi la ‘Mpanda Ngazi na Washika Ngazi’ (uk.95), Mpanda Ngazi anaonyesha tabia za baadhi ya wanasiasa ambao ni walaghai. Wanasiasa hao hutumia ahadi za uongo kupata mamlaka. Pindi tu wanapochaguliwa, huwasaliti wananchi ambao ni Washika Ngazi.

Mhimili mwingine ni kwamba nadharia hii husawiri matukio ya kihistoria. Katika shairi la ‘Ulifanya nini’ (uk.18), mshairi anatueleza namna kura zilivyopigwa vizuri kumchagua kiongozi lakini kura hizo zilibatilishwa mchana kwa kuibiwa. Katika shairi la ‘Mkuki kwa Nguruwe’ (uk.51), tunafahamishwa namna mkoloni alivyowasukumia wenyeji mateso ya kila aina. Wahusika hujitokeza vile vile kutekeleza matendo yao kwa njia ya kitabaka. Tabaka la chini, yaani wanyonge hujikakamua katika kujikomboa kwa kujipa mamlaka na nguvu za kiuchumi. Kwa hivyo, mhimili huu utatufaa zaidi kurejelea shairi la Mpanda Ngazi na Washika Ngazi (uk.95) katika kazi yetu.

Mhimili wa tatu wa nadharia ni kuwa jamii inasawiriwa kwa ukamilifu wake hivyo kuonyesha hatua ambazo jamii imepiga kimaendeleo. Mwisho ni kuwa nadharia hii inazingatia hali halisi ya jamii na inatumika kuelezea jinsi ambavyo jamii inavyoelekea kwenye usoshiolisti. Mihimili yote hii inatufaa katika uchanganuzi wa mada yetu.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Wataalamu mbalimbali wamefanya utafiti wao kuhusu siasa. Miongoni mwao ni pamoja na Mohamed ambaye amehakiki masuala ya kisiasa kwa kurejelea ushairi wake Kandoro (Mohamed, 2013). Ameongozwa na nadharia ya simiotiki, umaksi na ufeministi. Matokeo ya

utafiti wake yanaonyesha kwamba Waafrika walinyimwa nafasi ya kumiliki viti vingi katika baraza la wawakilishi katika kipindi cha ukoloni. Pia, utafiti wake Mohamed (2013) ulionyesha kwamba, Waafrika walinyang'anywa ardhi yao ambayo ilikuwa na rutuba na vile vile kunyimwa nafasi ya kupata elimu katika shule za umma na zile zilizofadhiliwa na kanisa na hivyo kuishia kuwa wachochole. Mawazo hayo ya Mohamed (2013) yamekuwa mwanga wa kupeleka mbele utafiti wetu. Utafiti wetu ni tofauti na wa Mohamed (2013) kwa kuwa sisi tumehakiki maudhui ya siasa na athari zake katika jamii kwa kurejelea diwani *Kaza Macho*.

Kwenye tasnifu yake, Mohamed (2013), anamrejelea Kitogo (2002) ambaye anasema kwamba Kandoro ametoa maelezo kuhusu maendeleo ya siasa katika awamu tatu: kipindi cha kutawaliwa na wakoloni, kipindi cha uhuru na baada ya uhuru. Mawazo haya ni muhimu katika utafiti wetu hasa kuchunguza ni kwa njia zipi siasa za baada ya uhuru zimeathiri jamii kwa kurejelea diwani ya *Kaza Macho*.

Omary (2011), amechambua siasa katika ushairi wa Kezilahabi. Matokeo ya uhakiki wake yamebainisha kuwa Kezilahabi anazungumzia masuala tofauti tofauti ya kisiasa katika diwani zake teule *Karibu Ndani* na *Dhifa* zilizochapishwa mwaka wa 1988 na 2008 mtawalia. Baadhi ya masuala ya kisiasa katika diwani ya *Karibu Ndani* ni pamoja na ugumu wa maisha wakati wa Azimio la Arusha na ukoloni mamboleo. Diwani ya *Dhifa*, imeibua masuala ya kisiasa kama vile siasa za kidemokrasia, siasa za vyama vya kisiasa, ufisadi miongoni mwa mengine. Mawazo ya Omary (2011) yametusaidia kuelewa kwa kina baadhi ya masuala ya kisiasa ambayo yameendelezwa katika utafiti wetu. Utafiti wetu ni tofauti na wa Omary (2011) kwa kuwa sisi tunahakiki maudhui ya siasa na athari zake katika jamii kwa kurejelea diwani ya *Kaza Macho*.

M'ngaruthi (2015), amefanya utafiti wake kuhusu usawiri wa mwanasiasa wa Afrika katika ushairi wa Kiswahili kwa kurejelea diwani tano zifuatazo: Utenzi wa *Uhuru wa Kenya* (Salimu A. Kibao, 1972), *Msimu wa Tisa* (Kithaka wa Mberia, 2007), *Sauti ya Dhiki* (Abdilatif Abdalla, 1973), *Chembe cha Moyo* (Alamin Mazrui,1988) na Diwani ya *Karne Mpya* (Ken Walibora, 2007). Utafiti wake ulikuwa na matokeo ambayo yalibainisha kuwa mwanasiasa katika kipindi cha kabla ya uhuru alijitolea kuukomboa umma. Baadhi ya wanasiasa walienda kinyume cha wenzao na kuonyesha vitendo vya ufisadi na usaliti. Baada ya uhuru, baadhi ya wanasiasa waliokuwa wakitetea maslahi ya umma waliendeleza tabia za mkoloni kwa kuwatesa na kuwakandamiza Waafrika. Mawazo ya M'ngaruthi (2015) ni muhimu kwetu kwa kuwa

yametusaidia kutolea maelezo ya kina nadharia yetu ya uyakinifu wa kijamii, kupitia maudhui ya usaliti na ufisadi na hivyo kusukuma mbele utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wetu ni tofauti kwa kuwa sisi tumehakiki maudhui ya siasa na athari zake kwa jamii tukirejelea diwani *Kaza Macho* ilhali yeye amehakiki usawiri wa mwanasiasa wa Afrika kwa kurejelea diwani tano zilizoorodheshwa hapo juu. Pili, M'ngaruthi (2015) ametumia nadharia mbili: ulimbwende na nadharia ya baada-ukoloni ilhali sisi tumeongozwa na nadharia moja, uyakinifu wa kijamii.

Gachukia (2005) ameangazia suala la uongozi wa kikabila na vyama vya kisiasa katika taifa la Kenya. Anaeleza kwamba Wakenya wanahitaji kutafakari endapo wataendelea kuongozwa na wanasiasa wanaojali makabila yao au maslahi ya vyama ambavyo viliwapeleka bungeni. Akirejelea historia ya Kenya kuanzia mwaka wa 1963, Gachukia, anasema kwamba kipindi hicho kilishuhudia viongozi ambao walijali maslahi ya Wakenya na kwamba uzalendo wa wanasiasa ulidhihirika kinyume na inavyojitokeza katika diwani, *Kaza Macho*. Utafiti wake Gachukia (2005) umetusaidia kuendeleza utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wa Gachukia unahitilafiana na wetu kwa kuwa Gachukia (2005) amechambua uongozi wa kikabila na vyama vya kisiasa katika taifa la Kenya ilhali sisi tumehakiki maudhui ya kisiasa na athari zake kwa jamii.

Chacha (1980), amehakiki kazi za Abdilatif Abdalla; Utenzi wa *Maisha ya Adam na Hawaa* (1976) na diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973). Ameangazia maudhui ya kisiasa kwa madhumuni ya kubainisha matatizo ambayo yalitokea katika nchi za Afrika baada ya kupata uhuru wa bendera. Utafiti wake ulikuwa na matokeo ambayo yalibainisha kwamba ushairi wa Kiswahili unaweza kutumika kama chombo cha kuwasilisha hisia za wananchi kuhusu ukatili wanaotendewa na viongozi. Miongoni mwa matatizo yaliyoshughulikiwa na Chacha ni pamoja na tamaa ya mali na ushindani wa kisiasa. Utafiti wake Chacha umechangia pakubwa kuendeleza utafiti wetu kwa kuwa baadhi ya matatizo yanayotokea katika tasnifu yake kama vile ukatili wa viongozi, yanaendelezwa na kukuzwa pia katika kazi yetu. Hata hivyo, kazi yetu ni tofauti na utafiti wa Chacha kwa kuwa sisi tumeangazia maudhui ya kisiasa na athari zake kwa jamii kwa kurejelea diwani *Kaza Macho.*

Katika utafiti wake, Waliaula (2009), anaeleza kwamba baada ya nchi ya Kenya kujinyakulia uhuru, upinzani ulianza kunyamazishwa na viongozi wa kisiasa. Waliojaribu kuikosoa serikali walitiwa mbaroni. Jambo hili lilichangia kuikuza fasihi iliyotungiwa magerezani. Waandishi

ambao walitiwa kizuizini kwa sababu ya kujaribu kuikosoa serikali ni pamoja na Alamin Mazrui, Ngugi wa Thiong'o na Abdilatif Abdalla. Mtafiti huyu ameonyesha dhuluma walizotendewa wananchi wakiwemo waandishi, jambo ambalo linajadiliwa katika utafiti wetu. Utafiti wetu unatofautiana na wa Waliaula kwa kuwa utafiti wake unalinganisha kazi za waandishi tofauti ilhali sisi tunahakiki kazi ya mshairi mmoja. Miongoni mwa kazi alizozichunguza Waliaula ni pamoja na *Mau Mau Detainee* (1961) ya J.M. Kariuki, *Sauti ya Dhiki* (1973) ya Abdilatif Abdalla, *Detained* ambayo ni manifesto ya Ngugi wa Thiong'o, *Mau Mau Author in Detention* (1988) ya Gakaara Wanjau na riwaya ya Wahome Mutahi, *Three Days on the Cross*. Waliaula pia, alizingatia kazi ambazo zilitungiwa gerezani zikiwemo zile za Kiingereza ilhali sisi tunatafiti mashairi yaliyotungiwa nje ya gereza. *Mau Mau Author in Detention* (1988) ni kazi iliyotungiwa gerezani lakini ikapata kuchapishwa baadaye. Mwandishi, Gakaara Wanjau analalama kuhusu kusahaulika kwa mashujaa waliopigania uhuru akiwa mmoja wao, Waliaula (2009:194). Katika tasnifu yake, Waliaula alihakiki masimulizi ya tenzi mbili ambapo alilenga kuelezea kuzuiliwa kwa wahusika kutokana na sababu za kisiasa. Alichunguza masimulizi ya utenzi wa Fumo Liyongo kutoka kwa jamii ya Waswahili katika maeneo ya Pwani ya Kenya. Pia, alichunguza masimulizi ya utenzi wa Sela na Mwambu kutoka jamii ya Bukusu, magharibi mwa Kenya. Kinyume na ilivyo katika utafiti wetu, Waliaula amehakiki kwa kujumlisha masimulizi ya tenzi ambazo zinahusu wahusika ambao wanaaminika kuwa mashujaa.

Adero (2005), amehakiki uwezo wa lugha katika matini ya siasa nchini Kenya. Utafiti wake ulikuwa na matokeo ambayo yalibainisha kuwa wanasiasa wanakuwa na mbinu mbalimbali za kuhimili mazungumzo yao ya kisiasa na kushawishi wananchi kuwapigia kura na kuwapa mamlaka. Matokeo vile vile yalionyesha kwamba baadhi ya wanasiasa waliishia kuwa maarufu kutokana na uwezo wao wa kutumia lugha. Utafiti wake Adero umetusaidia kuelewa dhana ya siasa na wanasiasa na hivyo kuishia kujenga msingi wa kukuza utafiti wetu. Utafiti wake Adero unahitilafiana na wetu kutokana na sababu kwamba Adero amehakiki lugha katika matini za siasa ilhali sisi tumehakiki maudhui ya kisiasa na athari zake kwa jamii. Kwenye utafiti wetu, tumeangazia pia mbinu za kisanaa ambazo zimetumiwa na mtunzi kuwasilisha maudhui hayo. Aidha, Adero ameongozwa na nadharia ya uchanganuzi usemi ilhali, sisi tunaongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamii.

Utafiti wa Haugerud na Njogu (1991) ulihusu mikutano ya kisiasa katika taifa la Kenya. Matokeo katika utafiti huu yalionyesha kwamba wanasiasa walitumia lugha ya kisiasa kwa

madhumuni ya kujinufaisha. Lugha ya wanasiasa hao huwa na ahadi na vishawishi vingi kwa wapigakura. Baada ya kuchaguliwa, wanasiasa hao huwasaliti wananchi kwa kukosa kutekeleza ahadi na hivyo huduma muhimu kukosekana katika jamii. Utafiti huu utatusaidia kupiga hatua katika kuangalia namna mamlaka wanayoyapata wanasiasa yanaathiri jamii. Utafiti wetu unatofautiana na wa Haugerud na Njogu kwa kuwa utafiti wao ni wa kiisimu ilhali wetu ni fasihi andishi ambapo tunarejelea diwani, *Kaza Macho*.

Bibiana (2014), amefanya utafiti wake kwa kuhakiki masuala ambayo yanahusu siasa ambapo anarejelea riwaya mbili za Shaaban Robert. Bibiana alikuwa na lengo la kutathmini masuala hayo ya kisiasa ambayo yanajitokeza katika riwaya za Shaaban Robert. Matokeo ya utafiti yalibainisha kwamba viongozi katika nchi za *Kusadikika* na *Kufikirika*, walijali maslahi yao na kupuuza yale ya jamii pana. Madhila ya aina tofauti tofauti k.v. ufisadi na dhuluma yamesababisha uchochole na ulitima katika jamii, jambo ambalo linazungumziwa kwa kina pia, katika kazi yetu. Hata hivyo, utafiti wetu unahitilafiana na ule wa Bibiana (2014) kutokana na sababu kwamba yeye anarejelea riwaya mbili: *Kufikirika* na *Kusadikika* ilhali sisi tunarejelea diwani, *Kaza Macho*. Aidha, utafiti wake umeongozwa na nadharia mbili: nadharia ya simiotiki na ile ya dhima na kazi ilhali sisi tunaongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamii.

Njogu (1987), ameshughulikia maudhui ya mapinduzi katika riwaya zifuatazo: *Utengano, Dunia Mti Mkavu* na *Asali Chungu.* Msomi huyu amebainisha kwamba matukio ya kihistoria huathiri jamii pakubwa. Katika tasnifu hii, mtafiti huyu ameangazia hali za kisiasa, kiuchumi na kijamii ambazo zilipelekea kutokea kwa mapinduzi ya Visiwani Zanzibar katika mwaka wa 1964. Tasnifu hii imetufaa sana katika kupeleka mbele utafiti wetu kutokana na sababu kuwa imedokeza kuhusu siasa mbaya, jambo ambalo linapigwa vita vile vile na Wamitilla (2014). Utafiti wetu unatofautiana na ule wa Njogu (1987) kwa kuwa tumeangalia kazi za nchi mbili tofauti. Njogu amehakiki maudhui ya mapinduzi akirejelea riwaya ya *Utengano*, *Dunia Mti Mkavu* na *Asali Chungu* ilhali sisi tunahakiki maudhui ya siasa na athari zake kwa jamii kwa kurejelea diwani, *Kaza Macho*.

Osango (2015), amehakiki ukombozi wa kisiasa na kiuchumi katika *Mkamandume*. Ametumia nadharia ya Uhalisia wa Kijamii. Katika tasnifu hii, msukumo wa waafrika kushiriki katika vita umechanganuliwa. Mtafiti huyu ameonyesha kwamba chanzo cha matatizo katika jamii hasa ya Zanzibar ni ubepari ulioanzishwa na wakoloni. Viongozi Waafrika waliukumbatia na hivyo

kusababisha hali ya maisha kuwa duni zaidi. Mawazo ya Osango (2015) yametupatia msingi wa kufahamu na kuelezea umaskini kama athari inayotokana na siasa mbaya. Tunatofautiana na utafiti wa Osango (2015) kutokana na sababu kuwa yeye amechambua ukombozi wa kisiasa na kiuchumi akirejelea riwaya ya *Mkamandume* ilhali sisi tunahakiki maudhui ya siasa na athari zake katika jamii tukirejelea diwani ya *Kaza Macho*. Osango anaongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamii ilhali sisi tunaongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamii.

Kwenye tasnifu yake, Rono (2013) amechambua fani na maudhui katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea ya Ken Walibora (2012). Baadhi ya maudhui aliyoyaangazia Rono ni pamoja na tamaa na uongozi mbaya. Nadharia zilizotumika hapa ni: Uhalisia wa Kijamii na Umuundo. Rono (2013), katika utafiti wake, alionyesha namna vijana walivyopigania kuondoa ukoloni mamboleo katika nchi yao ya Tomoko. Utafiti huu umetusaidia kusongesha mbele kazi yetu kutokana na kupata mwanga kuhusu dhana ya siasa na ukoloni mamboleo. Hata hivyo, utafiti huu wa Rono (2013) ni tofauti na kazi yetu. Katika utafiti wetu, tumechambua maudhui ya kisiasa na athari zake kwa kurejelea diwani, *Kaza Macho* ilhali yeye amechambua fani na maudhui kwa kurejelea riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*.

Kilonzo (2015), amechambua riwaya ya *Maisha Kitendawili* na kuhakiki maudhui ya siasa, uongozi, jinsia miongoni mwa mengine. Katika tasnifu hii, Kilonzo ameonyesha kwamba idadi kubwa ya wanawake katika Afrika hawajishughulishi na mazungumzo ambayo yanahusisha masuala ya kisiasa. Wanawake hao wamewaachia wanaume ambao wanajidai kuelewa siasa za nchi mbalimbali. Amebainisha dhuluma wanazotendewa wanawake kutoka kwa viongozi hao wa kisiasa. Kilonzo pia, ameeleza jinsi ambavyo mataifa mengi katika bara la Afrika yaliweza kuathirika na ukoloni. Mataifa hayo kwa mfano, yametawaliwa na maraisi wa kiume katika mifumo yao ya uongozi.

Utafiti huu umetufaa sana kwa kuwa maudhui ya siasa hasa uongozi mbaya yaliyoangaziwa ndiyo tumechambua. Hata hivyo, utafiti huu wa Kilonzo (2015) unahitilafiana na wetu. Mada yake ya utafiti ni, ‘ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*,’ ilhali sisi tunahakiki ‘maudhui ya kisiasa katika *Kaza Macho*. Kilonzo ametumia nadharia ya ufeministi wa kiafrika ilhali sisi tunaongozwa na uyakinifu wa kijamii.

**1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia.**

Watafiti mbalimbali wameweza kuitumia nadharia hii ya uyakinifu wa kijamii katika kazi zao. Miongoni mwao ni pamoja na: Muriithi (2013), Kiptum (2017) na Owallah (2013) miongoni mwa wengine.

Muriithi (2013), ameitumia kuhakiki 'athari za kidini' katika *Utenzi wa Rasi'lghuli* na kutambua kuwa utenzi huo una athari za kidini zilizo na uyakinifu katika jamii. Mawazo yake Muriithi yametusaidia kuhakiki diwani ya *Kaza Macho*, ambapo tumeangazia umaskini kama athari ya siasa mbaya katika jamii.

Kiptum (2017) pia, ameitumia katika kazi yake. Kiptum amechambua masuala makuu ambayo yanajitokeza katika Utenzi wa *Abdirrahmani na Sufiyani*. Kutokana na nadharia hii, Kiptum (2017) aliweza kudhihirisha kuwa dini ni suala kuu ambalo limezaa maudhui mengine k.v. usaliti, ndoa, mapenzi, ushujaa, vita, dhuluma na maridhiano. Maelezo yake yametufaa kabisa katika kuangazia masuala hayo ya usaliti, dhuluma na vita kwa mtazamo wa kisiasa tukirejelea diwani ya *Kaza Macho*.

Owallah (2013), ameongozwa na nadharia hii kuchambua maudhui teule. Baadhi ya maudhui hayo ni usaliti, maadili, dhuluma miongoni mwa mengine. Mawazo yake Ouma yametufaa zaidi kuelewa mihimili ambayo tumetumia katika utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wetu unatofautiana na wa Owallah (2013) kwa kuwa yeye amehakiki *Utenzi wa Nabii Isa* ilhali sisi tunahakiki diwani, *Kaza Macho*.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii, tumeonyesha njia za kuteua sampuli na kukusanya data. Tumeangazia vile vile, jinsi ya kuchanganua na hatimaye kuiwasilisha data hiyo. Sehemu hii imegawika katika vijisehemu vitatu vifuatavyo:

### 1.8.1 Njia za kuteua Sampuli

Tumetumia sampuli ya kimakusudi kama njia mojawapo ya uteuzi wa sampuli ambapo tunalenga kusoma kwa kina *Kaza Macho* ili kutambua maudhui ya kisiasa.

### 1.8.2 Njia za Kukusanya Data

Utafiti wetu umekuwa wa kimaktaba. Tuliingia maktabani ili kusoma kwa kina diwani, *Kaza Macho* kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ili kuwezesha uchambuzi wa mada yetu. Baada ya kusoma diwani, tulinukuu katika shajara sehemu muhimu ambazo zinalenga malengo yetu ya utafiti jinsi anavyodai Kothari 2008.

Pili, kuzuru maktabani ili kusoma tasnifu za wahakiki mbalimbali, majarida na vitabu vya waandishi tofauti tofauti. Kazi hizi zilitupatia mwongozo katika ufafanuzi wa utafiti ambao tumeshughulikia. Aidha, tulipekua mtandao na makala yanayohusu nadharia ili kupata uelewa zaidi wa mihimili iliyotumika kuhakiki maudhui ya utafiti wetu.

### 1.8.3 Uchanganuzi wa Data

Data ambayo imekusanywa imechanganuliwa na kutathminiwa kwa kutumia njia ya uchambuzi wa kimaelezo na ufafanuzi. Njia hii ya uchambuzi wa kimaelezo inamruhusu mtafiti kusoma shairi kwa kina na kuelewa maudhui na falsafa ya mwandishi. Mbinu hii huwa muhimu kwa kuwa humwezesha mtafiti kutoa maelezo zaidi kuhusu data ambazo zilikusanywa kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti.

### 1.8.4 Kuwasilisha Data

Matokeo ambayo yanatokana na uchanganuzi wa mashairi teule, yatawasilishwa kupitia maelezo na ufafanuzi kwa kurejelea diwani, *Kaza Macho*.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia mambo yafuatayo: utangulizi ambapo maelezo ya kimuhtasari kuhusu mada yametolewa. Tumefafanua dhana ya 'maudhui' na 'siasa' kulingana na wataalamu mbalimbali. Tatizo la utafiti vile vile limeangaziwa. Lengo kuu la utafiti limeangaziwa. Lengo hilo ni kuchanganua namna suala la siasa linavyojitokeza katika diwani ya *Kaza Macho*. Tumeorodhesha maswali ambayo yananuiwa kujibiwa ili kuwezesha kukamilika kwa malengo ya utafiti.

Tumeeleza sababu ambazo zimetufanya kuchagua mada hii. Kuhusu upeo na mipaka, tumesoma diwani, *Kaza Macho* na kuchambua mashairi yanayoangazia masuala ya kisiasa. Nadharia ya Uyakinifu wa Kijamii na mihimili yake imefafanuliwa kama msingi wa kuongoza utafiti wetu.

Tumegusia mchango wa wataalamu mbalimbali kuhusiana na mada yetu na kuonyesha jinsi ambavyo kazi zao zinatofautiana na mada yetu. Tumebainisha njia ambazo tumetumia kuteua na kukusanya data. Mwisho, uchanganuzi wa data pamoja na uwasilishaji wake umeelezwa. Tumeangazia uchanganuzi wa maudhui ya siasa katika sura inayofuata.

# SURA YA PILI:
# UCHANGANUZI WA MAUDHUI YA SIASA

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia na kuwasilisha maudhui ya siasa kama yanavyojitokeza katika diwani ya *Kaza Macho*. Tumefanya hivyo kwa minajili ya kutimiza madhumuni na lengo kuu la utafiti wetu. Aidha, uchunguzi wetu umeongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamii ambayo iliasisiwa na Stalin mwaka wa 1917. Tumefanya uchanganuzi wa maudhui baada ya kuisoma diwani yenyewe kwa mapana na kuelewa maudhui na vipengele vyake.

## 2.1 Maudhui ya Siasa

Kwa mujibu wa Kilonzo na Masaku (2018) siasa ni mfumo wa kijamii ambao unahusu matumizi ya sheria katika kufanya maamuzi ya kiutawala katika asasi mbalimbali za kijamii. Vilevile, wanaeleza siasa kama itikadi ambayo hutumiwa na jamii kama nyenzo ya kuendeleza asasi mbalimbali za kijamii kama vile uchumi, siasa, dini miongoni mwa nyingine. Kutokana na maelezo ya wasomi hawa, hatuna budi kusema kuwa siasa ndiyo asasi kuu katika muundo msingi wa jamii yoyote kwani ndiyo hutumiwa kuziendeleza asasi zingine zote za jamii.

Siasa ni shughuli ya kijamii ambayo si rahisi kutolewa maelezo kwani ndani yake imebeba mambo mengi. Siasa ni asasi kuu ya kijamii ambayo mbali na kuleta migongano ya kijamii pia huleta mshikamano wa wanajamii. Hata hivyo, hii haina maana kuwa kila shughuli inayofanywa katika jamii ni ya kisiasa bali ina maana kuwa siasa hutumika kama nyenzo ya kutekelezea shughuli mbalimbali za kijamii. Siasa inahusisha ushindani baina ya viongozi kwa kusudi la kujitafutia umaarufu katika jamii. Katika ushindani huu panaibuka maoni kinzani ambayo husababisha jamii kugawika kwa misingi ya kitabaka.

Jamii hutegemea siasa kuwa suluhisho la matatizo yanayoikumba kupitia kwa viongozi wanaochaguliwa na kupewa nyadhifa mbalimbali za kimamlaka. Baadhi ya viongozi huwa na tamaa ya mali na hivyo kuweka matakwa yao mbele badala ya kutatua matatizo ya kijamii yaliyoko. Matokeo ya hali hii ni jamii ambayo inabaki nyuma kimaendeleo.

Kadri jamii inavyobadilika kutokana na utandawazi ndivyo siasa inavyobadilika. Mabadiliko haya yanatokana na mwingiliano wa watu walio na tamaduni mbalimbali na pia hali tofauti za kiuchumi. Dhana ya siasa wakati wa wataalamu kama vile Aristotle ilihusu wanajamii

kusaidiana katika kutatua matatizo mbalimbali yaliyowakumba; tofauti na ilivyo sasa ambapo siasa ni ya kudhihirisha ubeberu, ubinafsi na tamaa ya viongozi. Hali hii imepelekea wanajamii kutowaamini viongozi wao na pia kutozingatia sera zao wakati wa uchaguzi. Katika diwani ya *Kaza Macho,* K.W. Wamitila ameangazia maudhui ya siasa yafuatayo:

### 2.1.1 Uongozi wa Kiimla.

Uongozi ni cheo ambacho mtu hupewa na jamii kwa lengo la kusimamia kazi au shughuli fulani ya kijamii. Haya ni kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili iliyochapishwa mwaka wa 2015. Uongozi kwa hivyo huwa mamlaka anayopewa mtu kwa ajili ya kuwaongoza watu au kundi fulani katika jamii. Watu ambao wanaongozwa huwa ima wameitikia kuongozwa kupitia kwa kura zao au kupitia kwa maamuzi kutoka kwa watawala ambao tayari wapo mamlakani. Katika hali ambapo wanajamii wenyewe huchagua viongozi wao kupitia kura, jamii au nchi hiyo husemekana kuwa inaongozwa kwa misingi ya kidemokrasia. Kwa upande mwingine, jamii ambayo suala la uongozi haliamuliwi kupitia kwa kura ya mwananchi husemekana kuwa inaongozwa kiimla. Uongozi mara nyingi hutoa dira ya maendeleo kwa jamii kutegemea kama ni uongozi mzuri au mbaya.

Uongozi mbaya ni ule ambao hauwaletei wananchi maendeleo kupitia sera nzuri. Uongozi mbaya huwa kama nyenzo ya kutopatikana kwa maendeleo katika jamii au taifa. Viongozi wasiofaa huchangia pakubwa katika kuzoroteka kwa maendeleo katika jamii. Sampuli hii ya viongozi mara nyingi huwa hawashirikishi wananchi na kuwashauri juu ya maendeleo ya nchi. Viongozi hao huongozwa na tamaa na ubinafsi hivyo kushiriki katika vitendo vya kupora rasilimali za nchi yao. Isitoshe, ahadi za uongo hutolewa ili kuwapumbaza wananchi kuwapigia kura. Wakati mwingine kunashuhudiwa visa vya ukiukaji wa haki za kibinadamu. Uongozi wa aina hii huendesha sera za serikali kwa njia isiyokuwa wazi.

Kwa upande mwingine, uongozi mzuri unahusu viongozi ambao huweka maslahi ya wananchi mbele wakati wanatekeleza shughuli nzima ya utawala. Baadhi ya maslahi haya ni kama vile kuanzishwa kwa miradi ya kuwafaidi wananchi ikiwemo hospitali na shule, kuzilinda haki za wanajamii wote kwa usawa, kuwawakilisha wanajamii vyema katika vikao rasmi vya serikali kama vile bunge miongoni mwa masuala mengineyo.

Suala hili la uongozi mbaya linadhihirika kwa uwazi katika diwani ya *Kaza Macho* kupitia kwa sauti ya mtunzi ambayo inamulika maovu ya viongozi hasa wa nchi za Afrika kwa njia ya tashtiti. Mashairi mengi katika diwani hii yanadhihirisha dhuluma za watawala kwa watawaliwa. Kwa mfano, katika shairi la 'Kipofu na Kichaa' (uk.78), mwandishi anatuchorea taswira ya ujinga wa wanajamii ambao humchagua kiongozi ambaye hawamfahamu vyema na baadaye kuanza kulalamika kiongozi huyo anapoanza kuwanyanyasa. Haya yanathibitishwa katika kifungu cha pili mstari wa nane na tisa.

"Ikisemwa mtaani, huyu ni njemba fanani,
Na apewe usukani, aongoze kijijini."

Kwa tashtiti mwandishi anaeleza kuwa ki pofu na kichaa ndio walipinga kuchaguliwa kwa kiongozi huyo na hata kuwatahadharisha wanajamii hao pasi na kusikizwa. Kupitia kwa kichaa na kipofu, mtunzi anajaribu kuonyesha jinsi wanajamii wanavyoongozwa na ubinafsi na tamaa wakati wa kampeni na kukosa kutilia maanani sifa za yule wanayemchagua. Wanajamii wengi huhadaiwa na wanasiasa kwa kutumia pesa kidogo, kununuliwa chumvi au sukari, leso au kanga, pombe, na kupewa ahadi za uongo. Hata hivyo, wapo wachache ambao husimama kidete na kukataa hadaa za namna hii ambazo matokeo yake ni uongozi usiomjali mwananchi. Watu kama hawa ndio mtunzi anawarejelea kama vichaa na vipofu ambao maoni yao hayasikilizwi wala kuzingatiwa na yeyote kama inavyodhihirika katika kifungu kifuatacho:

"Tuliambiwa yakini, kuwa huyu hayawani,
Tukacheka midomoni, kichaa ajua nini?
Kisha kipofu jamani, kasema yake jamani,
Tukamba kaona lini, huyu naye ajuani?
Kumbe sisi ndio nyani, tuna macho hatuoni,
Tuna akili vichwani, hatutumii lakini" (kifungu cha 12 uk.83).

Nchi zinazoendelea hasa za bara la Afrika, baadhi ya wanasiasa hujitokeza katika uwanja wa kisiasa bila kuwa na sera nzuri au mipango kabambe ya kuongoza jamii. Wanasiasa wa sampuli hii kwa kawaida huongozwa na tamaa ya kujichumia mali ya umma na kujitajirisha bila kumjali mnyonge au mwananchi wa kawaida.

Katika shairi la 'Ina Nini?' (uk.71), mwandishi anauliza sababu inayowafanya watu wengi kama vile madaktari, wafanyabiashara, maprofesa miongoni mwa wengine kuacha kazi zao na

kujiingiza katika kinyang'anyiro cha uongozi. Mtunzi anashangazwa na tabia za watu wasomi wenye hadhi na madaraka kuacha kazi zao na kujitoma katika ulingo wa siasa. Katika ubeti wa nne na wa tano, anahusisha suala hili na dini kwa kutaka kufahamu sababu inayowafanya hata wahubiri kanisani na mashehe msikitini kuacha kazi zao na kuingia katika siasa (uk.71).

Kupitia kwa mfano huu ni bayana kuwa wengi wanaoingia katika siasa huwa na maazimio ya kujiboresha kimaisha kwa kuongeza idadi ya kipato chao. Hii ina maana kuwa kwa mwanasiasa kilicho muhimu ni pesa anazopata na wala sio kazi anayopewa na mwananchi ya kumwakilisha katika vikao vya serikali na pia ugavi wa rasilimali za umma.

Katika ngonjera ya 'Mpanda Ngazi na Washika Ngazi' (uk.95), suala hili la uongozi linaelezwa kwa jazanda. Mwandishi anatumia Mpanda Ngazi kuashiria wanasiasa wanaowaomba wananchi kura kwa ahadi kuwa wakishachaguliwa watawasaidia. Viongozi hawa wanawashawishi wananchi na kuwahadaa punde tu wapatapo uongozi, watayatatua matatizo yao. Ajabu ni kuwa baada ya wao kupata madaraka, wao hujitenga na kuwadharau wananchi hao hao waliowachagua kama inavyodhihirika kupitia mfano ufuatao katika ubeti wa 17:

> …"Iweje leo fulani, tukupandishe,
> Utunde yalo mtini, na kuyatia tumboni,
> Na ganda watupa chini, ukitucheka kinywani,
> Mti wetu kijijini, wala si wako fulani."

Kupitia mfano huu mtunzi anaonyesha jinsi viongozi wanavyojinyakulia mali ya umma na kuitumia kujiboresha au kujiendeleza kibinafsi bila kumjali mwananchi. Kinachofuata ni viongozi hawa kujitafutia makao ya kifahari na kuhamia huko ili wasisumbuliwe na wananchi ambao mahitaji yao ni mengi.

Wananchi wamekosa matumaini kwa wanasiasa wao. Uhuru waliopata ni wa bendera tu. Wanaofaidika ni wanasiasa pamoja na vibaraka wao ikiwemo mawaziri. Kupitia shairi la 'Uhuru' kifungu cha kwanza msitari wa tatu, mshairi anasema kwamba, 'uhuru ni uraibu katika domo kaya la wanasiasa' (uk.15). Kauli hii inadhihirisha kwamba wanasiasa wameshindwa kuwatatulia wanajamii matatizo yao kupitia sera nzuri. Sera zilizoko badala ya kuyainua na kuboresha maisha ya wananchi, zimetumika kuwakandamiza wananchi. Katika shairi la 'Uhuru' (uk.15) mtunzi anaeleza yafuatayo kuihusu sera:

> "Sera

Imekuwa kisawe cha ufisadi,
Limekuwa neno la mashavu kuyavimbisha,
Nta ya kuyakwamizia maisha ya nchi,
Ngome ya kuwazingira wenye mamlaka,
Neno la kuhalalisha ukwepuzi mchana" (kifungu cha pili).

Mfano huu unaonyesha wazi kuwa viongozi wengi katika mataifa yanayoendelea hawana sera yoyote bora ambayo wanaweza kujitambulisha kwayo kama sio ufisadi. Ufisadi umekuwa jambo la kuzungumziwa kila siku kutokana na tamaa ya viongozi wetu. Viongozi hawa hawana maono yoyote ya kuendeleza nchi kimaendeleo au kuziboresha kiuchumi. Hata hivyo, viongozi hasa walio mamlakani huwa hawaoni aibu yoyote katika kuzisifu na kuzipigia debe sera ambazo zimepitwa na wakati. Kauli hii inathibitisha sifa za wanasiasa wanaoongoza jamii kuwa ni wanyonyaji. Wanapenda ulafi na kusifu ubwege kama inavyojitokeza katika shairi la Ushamwona (kifungu cha 4 uk.30).

### 2.1.2 Ukiukaji wa Haki za Kibinadamu

Kifungu cha 26 cha Katiba ya Kenya 2010 kinatambua kwamba kila binadamu ana haki ya kuishi maisha ambayo yamelindwa kutokana na dhuluma zozote za kijamii. Kifungu cha 51 vile vile kimeeleza haki ya watu wanaozuiliwa na wale ambao wamefungwa kwamba wanapaswa kupata huduma zote za kimsingi na pia kuhakikishiwa usalama bora. Wafungwa kama binadamu wengine wote wana haki ya kupata mavazi bora, lishe bora na makazi bora. Katika diwani ya *Kaza Macho,* mtunzi amezungumzia suala la ukiushi wa haki za kibinadamu kama ifuatavyo:

#### 2.1.2.1 Wizi wa Haki ya Mpiga Kura

Katika nchi zenye demokrasia shirikishi, watu ambao ni wachache hupewa dhamana sawa na walio wengi katika uwakilishi wa jamii katika kutekeleza na kufanya maamuzi. Watu hao wachache huchaguliwa na wengi kupitia njia ya demokrasia iliyo huru na haki kwa kufuata katiba ya taifa hilo. Katika taifa la Kenya kwa mfano, raisi wa taifa, magavana, maseneta, wabunge wa bunge la taifa na wale wa majimbo na wawakilishi wa akina mama bungeni huwakilisha wananchi wao kwa lengo la kuleta maendeleo na vile vile kuishauri serikali juu ya maendeleo hayo.

Sauti ya wapiga kura haizingatiwi. Wanapiga kura vizuri kumchagua kiongozi wao lakini kura hizo hubatilishwa. Kulingana na wanasiasa hao, wapiga kura huonekana kutokuwa na akili razini endapo wamemchagua kiongozi ambaye hatakikani na wenye nguvu. Katika shairi la Ulifanya nini (uk.18), wapiga kura wanaibiwa haki yao ya kuchagua kiongozi. Baada ya kura kupigwa mchana peupe, kura hizo zinabatilishwa na kupewa mshindi ambaye hafai kuliongoza taifa. Wanaobadilisha kura hudai kwamba wapiga kura hao hawana akili na kwa hivyo hawakufahamu walichokuwa wakifanya mwanzoni. Kutokana na vitisho vyao, viongozi hao huwalazimisha watu kubadili ukweli na kusema uongo kama inavyojitokeza katika mfano ufuatao:

"unaikumbuka siku
Ya kura,
Iliyopigwa mchana,
Iliyopigiwa foleni
Iliyobatilishwa mchana,
Iliyoshindwa na mshinde?" (kifungu cha 1).
Unaikumbuka siku,
Ilipodaiwa huna akili,
Iliposemwa hukujua kabla,
Ulichokuwa ukikifanya?" (kifungu cha 2 uk.18).

Mtunzi ametumia maswali ya balagha kumkejeli mpiga kura ambaye baada ya kushiriki katika uchaguzi na kumchagua kiongozi ampendaye, anashawishika kukubali matokeo ya uchaguzi ambayo tayari yamebatilishwa. Mshairi analinganisha kitendo hiki na mtu ambaye amezuzuliwa kiasi cha kushindwa kuona ukweli. Mpiga kura huyo analazimika kuitikia matokeo hayo kwa sababu ya kutishiwa maisha.

Wanasiasa hao wamewatia wananchi uoga si haba na kuwafanya kukataa ukweli na uaminifu na badala yake kuukubali uwongo, wizi na mauaji. Jamii imeonekana kukumbatia uwongo badala ya kuitikia kuongozwa kwa ukweli. Kwenye jamii hii, uaminifu umeharamishwa na kuonekana kama kitu kisichopendeza. Wizi umehalalishwa na kufanywa mchana peupe. Wizi huu unafanyika katika afisi mbalimbali iwe ni za umma au ni za mashirika ya kibinafsi. Watu wema wamebadilika na kuwa majangili kama inavyodhihirika katika shairi la 'Kibinimethali' (uk.16).

"Wizi

Umegeuka halali, mchana umesimika,

Mwema akawa jangili, jamaa wa kuepuka,

Mroho kawa mithili, ya mtu wa kutajika,

Wizi dira kushika, mauaji si kiroja" (ubeti wa 4).

Wanaoibia nchi yao hukimbilia maabadani wanakotoa sadaka au mchango kwa lengo la kuficha maovu yao. Watumishi wa Mungu hufumbwa macho ya kuona maovu hayo kupitia hela hizo. Dini badala ya kukemea na kukashifu matendo hayo, inatumika kuhalalisha wizi wa kimabavu kama inavyodhihirika katika shairi la 'Uhuru' uk.15.

"Dini

Imekuwa liwazo la wadidimiao katika dhiki,

Imekuwa kimbilio la wapiga nchi kabari,

Imekuwa sherehe ya kuhalalisha bakuzi,

Imekuwa pendekezo la wakuu wa nchi" (kifungu cha 4).

Kauli hii inathibitisha ya kwamba unafiki umejaa na kutamalaki maabadani hasa miongoni mwa watumishi wa Mungu. Shairi la 'Siku ile Kanisani' (uk.48) linaibua taswira kamili ya mambo ambayo yanaendelea maabadini. Machoni pa wahubiri, wenye nguvu hujitokeza kama mashujaa wa kustahiki. Mkondo wa mahubiri hubadilika ghafla pindi tu wanasiasa wanaingia kanisani. Wanakoma kukemea maovu na kufundisha maadili kwa waumini wao. Maombi ya wahubiri hao hujaa sifa kem kem wanazomiminiwa wenye nguvu au majitu kwa kulinganishwa na simba ambaye ni mcha Mungu kama inavyojitokeza kupitia mfano huu:

'Maombi,

Mhubiri hakuomba, asilani,

Lakini 'liimbaimba, kwazo kani,

Kumsifu huyo simba, alo ndani…' (kifungu cha 13 uk.49).

Katika shairi la 'Mgonjwa' (uk.19), mshairi ametumia neno mgonjwa kijazanda kutuchorea taswira ya masikini ambaye ameishi miaka mingi akiwa na matumaini kwamba maisha yake yataboreshwa na viongozi waliochaguliwa. Ajabu ni kwamba akiba ya mgonjwa huyo inaporwa hadharani na majambazi ambao wanaitumia kujenga makasri kama inavyojitokeza katika shairi hilo la Mgonjwa, kifungu cha pili:

"Nimeiona akiba yake;

Ikiporwa na majambazi,

Ikihamishiwa kuzimu,

Ikijenga na makasri,

Ikitimbwa kwa ghasia,

Isimfae hata chembe."

Licha ya Kipofu na Kichaa kutahadharisha kuhusu kumchagua kiongozi aliyekuwa na maadili ya kutiliwa shaka, wapiga kura waliyatia masikio yao nta na kumchagua kiongozi huyo. Wapiga kura hao wanajutia uamuzi waliofanya wanapogundua kwamba aliyechaguliwa ni mwizi hodari. Anaiba ardhini na hata maporini kama inavyojitokeza kwenye shairi la 'Kipofu na Kichaa' (uk.84). Katika shairi la 'Jikanye' (uk.23), mwananchi anahitajika kuucheka ujinga wake sio tu kwa kumwaamini jambazi na kumshangilia mlanguzi pia kwa kumpa zawadi pwaguzi na kumtuza mwizi.

"Cheka

Ucheke ujinga wako wa kumwamini jambazi,

Ucheke ujuha wako wa kumhongera mlanguzi,

Ucheke ubwege wako wa kumtunuku pwaguzi,

Ucheke upumbe wako wa kumzawadi mwizi" (ubeti wa 2 uk.23).

**2.1.2.2 Haki ya Kupata Lishe Bora.**

Ni haki ya kila binadamu kupata lishe bora ambayo itamuwezesha kuwa na afya nzuri na hatimaye kupelekea kuwepo na jamii ambayo inawajibika katika kuendeleza shughuli za kijamii k.v siasa, kilimo, biashara, n.k. Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi ambavyo haki hii muhimu ya kupata lishe bora imehujumiwa. Katika shairi la 'Niko Hapa' (uk.113) kwa mfano, mtuhumiwa anapewa chakula kibaya ambacho kinahatarisha maisha yake. Chakula hicho kinamnyima usingizi wa kulala.

"Niko hapa

Nikila chakula kiso chakula,

Na kuwa macho ninapolala,

Kwa sababu nilitetewa,

Na wakili aliyeshindwa,

Kunielewa na ambaye,

Aliyemtuma simjui ni nani" (kifungu cha tatu).

Kupitia shairi la 'Kichekesho cha Historia' (uk.74) mshairi anaeleza masaibu wanayoyapitia vijana wa kuranda randa mitaani ili kupata chakula. Inabidi vijana hao wawe wa kuomba omba angalau kutia tonge kinywani huku wanasiasa wakionekana wakiwa na chakula tele ambacho kimejaza matumbo yao kama inavyodhihirika katika uk.74-75.

**2.1.2.3 Haki ya Kupata Makazi Bora.**

Makazi wanayoishi watu yamefumbikwa na giza. Viongozi waliopo hawajachukua hatua yoyote kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata makazi bora. Katika shairi la 'Niko Hapa' (uk.113), haki ya mtuhumiwa kupata makazi bora imekiukwa. Mazingira ya chumba wanamozuiliwa wafungwa ni ya kutiliwa shaka na vile vile ya kuhatarisha maisha. Chumba hicho kinamithilishwa na magofu na wanaoishi humo ni, "wenye uhai-wafu" (kifungu cha kwanza uk.113). Katika shairi la 'Tazama,' kuna umma ambao umetaabika na kulia kwa sababu ya kukosa pahali pa kulala (uk.14). Baadhi ya viongozi ambao wana nguvu katika jamii wameonekana wakinyang'anya maskini makazi yao japo ni duni kama inavyojitokeza katika shairi la Utenzi wa Ndovu na Mja (uk.106). Aina hii ya viongozi hawajali vilio vya wananchi muradi tu wao wametimiza haja zao.

**2.1.3 Usaliti**

Mataifa mengi katika bara la Afrika yalikuwa chini ya himaya ya wakoloni. Waafrika walijitolea kupigania uhuru wao ili kujitawala. Baadhi ya waafrika walijiunga na wakoloni hao katika kuwasaidia kupiga na kuwadhulumu waafrika wenzao wakiwa na matumaini kwamba wangepatiwa vyeo au kuzawadiwa na serikali hizo za wakoloni. Kitendo hiki kilidhihirisha usaliti mkubwa kwa waafrika.

Baada ya waafrika kujinyakulia uhuru wao, waliwachagua viongozi wao katika serikali ili kujitawala. Walifanya hivyo wakiwa na imani kwamba shida zao zikiwemo ukabila, ujinga, ubaguzi, umaskini, n.k. zingefikia kikomo. Viongozi hao walitarajiwa kuwa katika mstari wa mbele kushirikiana na wananchi kuleta maendeleo ya haraka katika jamii kupitia sera nzuri. Kinyume na matarajio ya wengi, viongozi hao walijitia hamnazo na kuwasahau waafrika wenzao wakiangamia katika lindi la umaskini.

Waliongozwa na ubinafsi na tamaa katika kujitajirisha kwa kujilimbikizia rasilimali za umma. Tendo hili lilidhihirisha usaliti kwa wapiga kura pia. Wanasiasa hutoa ahadi za miradi mbalimbali ambayo watatekeleza endapo watachaguliwa na wananchi. Pindi tu wanapochaguliwa, viongozi hao huwasaliti wananchi kwa kuvunja ahadi zao.

Wakati wa kampeni, wanasiasa hao huahidi kuinua uchumi na kuboresha miundo msingi. Jambo la kushangaza ni kuwa baada ya kuchaguliwa, ahadi hizo husahaulika. Katika shairi la Mpanda Ngazi na Washika Ngazi, wanasiasa wanajinyenyekeza na kuahidi maendeleo kwa wapiga kura katika kuomba kura. Wapiga kura wanawachagua baada ya kushawishika. Baada ya kuchaguliwa, viongozi hao wanawaona wapiga kura kuwa watu wajinga wanaostahili kuteseka. Wanawasaliti wapiga kura kwa kuwaonyesha kiburi kama inavyojitokeza katika ubeti ufuatao:

…"Sasa kwamba u mtini, kiburi kimo kichwani,
Kumbuka kuwa lakini, utajashuka mwishoni…
Iweje leo fulani, tukupandishe mtini,
Utunde yalo mtini, na kuyatia tumboni,
Na ganda watupa chini, ukitucheka kinywani,
Mti wetu kijijini, wala si wako fulani" (ubeti wa 16 uk. 98).

Viongozi wasaliti wamegeuza uzalendo kuwa uhaini na wema kuwa uovu kama inavyodhihirika katika shairi la 'Kadhia ya Jana' (uk.21). Viongozi wanapochaguliwa katika jamii, inatarajiwa kwamba watekeleze wajibu wao. Viongozi hao waweze kuwasaidia wananchi kuunganisha uwezo na nguvu zao, kuratibu na kusimamia shughuli huku wakiwaelekeza njia mwafaka ya kufikia malengo yao. Viongozi katika mataifa mengi ya bara la Afrika walipuuza majukumu yao. Wanasiasa hao hutumia afisi zao kuyajaza matumbo yao. Katika shairi la 'Kwa nini' (uk.6), mshairi analalamika jinsi ambavyo uhuru umegeuzwa ili kuwafaidi watu wachache ambao wanajaza matumbo yao na kunenepa kama nguruwe.

…"Uhuru unapogeuzwa,
Ulaji wa matumbo makubwa,
Ya kuwashinda wanayoyamiliki.
Kuyabeba" (uk.6).

Usaliti huu unadhihirika wazi katika shairi la 'Kipofu na Kichaa' (uk.78). Mja aliyetaka kupewa nafasi ya kuongoza alijiwasilisha kwa jamii kama kiongozi atakayeikomboa jamii hiyo

iliyogubikwa na giza la umaskini. Alipopewa nafasi ya kuongoza, aliwasaliti wananchi waliokuwa na matumaini makubwa kwake. Kiongozi huyo aligeuka kuwa jambazi. Aliwaibia wananchi migodi yao na kuwaacha maskini zaidi. Mitaani, aliwaharibu mabinti za watu kwa kuendeleza ubakaji (uk.80).

### 2.1.4 Ufisadi

Kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015), ufisadi ni ile tabia mbovu inayoharibu hali ya maelewano miongoni mwa waja kwa kutenda mambo yanayowagombanisha au yatakayowagombanisha. Pia, ni kitendo cha kufanya wizi au ubadhirifu wa mali ya umma kwenye dhamana yako. Ni tendo la kumdhulumu mtu kimaksudi kwa kumnyima haki yake. Ufisadi vile vile ni matumizi ya madaraka katika afisi za kiserikali au za kibinafsi kwa lengo la kumfaidi mtu binafsi au kundi maalum la watu. Ni ile hali ya kutoa au kupokea hika jamii, ufisadi hujitokeza katika viwango viwili tofauti. Kimoja ni kiwango cha chini kinachohusisha mwananchi wa kawaida akiwa katika shughuli zake za kila siku. Kiwango kingine cha ufisadi ni kile kinachohusisha mabwanyenye au watu wenye nguvu katika serikali. Hiki ni kiwango cha juu cha ufisadi. Viongozi wanaoshiriki, katika ufisadi mara nyingi huongozwa na tamaa, ulafi na ubinafsi.

Udhaifu wa sheria za nchi mara nyingi umechangia kuendeleza janga hili la ufisadi. Walio na mamlaka wamefahamu kwamba hamna hatua yoyote inayoweza kuchukuliwa dhidi yao. Viongozi huendeleza ufisadi kutokana na sababu kuwa wananchi wamepuuza jambo hili. Hawapigi makelele au kulalamika hadharani.

Janga hili la ufisadi limeathiri pakubwa bara la Afrika. Viongozi wakuu serikalini wanaendeleza kashfa hii na kusababisha kupotea kwa mamilioni ya fedha. Uchumi wa nchi umeharibika na wananchi kusalia kuishi katika maisha ya ulitima. Gazeti la *The Standard* tarehe 11 Novemba mwaka wa 2020, liliripoti visa vya ufisadi wa mabilioni ya pesa kutoka kwa serikali ya Kenya. Kwenye gazeti hilo, iliarifiwa kuwa afisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Kuendesha Mashitaka nchini Kenya (ODPP) ilirekodi kesi zinazogharimu shilingi bilioni 224 kuhusisha maafisa wa ngazi za juu serikalini chini ya miaka mitatu pekee iliyopita. Kesi 53 za tuhuma za ufisadi zinahusisha mawaziri saba na makatibu wa kudumu wa wizara, magavana 11 na maafisa wakuu katika serikali za kaunti, wakurugenzi 22, wabunge saba miongoni mwa wengine. Wanaotuhumiwa na njama hii ya ufisadi ni pamoja na: Aliyekuwa waziri katika wizara ya fedha bwana Henry

Rotich, ambaye amekabiliwa na mashitaka ya shilingi bilioni 63 kuhusu ujenzi tata wa mabwaga ya Kimwarer na Aror. Aliyekuwa Waziri wa michezo bwana Hasan Wario anapambana na kesi mahakamani alikoshitakiwa kuvuja shilingi milioni 55 za Rio Olimpiki.

Magavana wengine ambao kesi zao za ufisadi hasijakamilika mahakamani ni: Mike Mbuvi Sonko (aliyekuwa gavana wa kaunti ya Nairobi), Moses Lenolkkulal (Samburu), Muthomi Njuki (Tharaka Nithi), Ali Korane (Garissa), Okoth Obado (Migori) na aliyekuwa gavana wa Kiambu bwana Ferdinand Waititu. Inadaiwa pia kuwa kuna baadhi ya maafisa wakuu serikalini waliofaidika na msaada wa mabilioni ya pesa za kusaidia kupambana na janga la Korona nchini Kenya katika Mwaka wa 2020.  Ufisadi unajitokeza katika diwani kama ifuatavyo:

Ufisadi unaendeshwa katika vituo vya kurekebishia tabia. Hongo inaitishwa hadharani. Wahalifu hukwepa mkono wa sheria kupitia njia hii na wakati mwingine, wasiokuwa na hatia hulipa gharama kwa kusingiziwa kufanya uhalifu. Katika shairi la 'Niko Hapa' (uk.113), mtuhumiwa anatumikia kifungo kwa kukosa hela za kuhonga ili aweze kufunguliwa lango usiku (uk.114).

…'Niko hapa,
Ninapoitwa kwa nambari,
Jina lilipokuwa sifuri,
Kwa sababu nilipungukiwa,
Na hela za kumpenyezea,
Aliyeahidi kunifungulia,
Lango usiku wa giza totoro' (kifungu cha 4).

Katika shairi la 'Kwa Nini' (uk.6), swala hili la ufisadi limedhihirika. Mshairi anaeleza jinsi ambavyo watu wachache wamefaidika kutokana na kushiriki katika sakata hii ya ufisadi. Watu hao wameyajaza matumbo yao na kunenepa kama manguruwe. Wananchi wameachwa wakiteseka. Ufisadi huu umewanyima wananchi wa kawaida raha ya kusherehekea uhuru wao.

Katika shairi la 'Mwanasiasa' (uk.11), mwanasiasa wa bara la Afrika amesawiriwa kama mtu asiyeaminika tena. Amelinganishwa na kinyonga kutokana na kuwa na hulka ya kubadilika badilika. Badala ya kuwa mzalendo, amegeuka kinyonga anayejilimbikizia mali na kukosa kutekeleza majukumu yake. Ufisadi umekuwa sera ambayo imetumika na hao wanasiasa kujiendeleza kiuchumi na kuyakwamiza maisha ya jamii kama inavyodhihirika katika shairi la 'Uhuru' (uk.15).

Taasisi mbalimbali za serikali zimeathirika kutokana na kashfa za ufisadi. Katika shairi la 'Chini ya Mgunga' (uk.53) kwa mfano, shule hazina pesa za kujenga madarasa mengine. Tamaa iliwasukuma wanasiasa kufilisisha hazina ya fedha iliyotengewa ujenzi huo. Viongozi ambao walistahili kusimamia na kuendesha miradi hiyo ya ujenzi walipora hela.

> 'Nakumbuka kuwa shule haikuwa na pesa,
> Za kujenga madarasa mengine,
> Serikali nayo ilishatobokwa na mifuko,
> Mapeni yakaanguka njiani,
> Kwenye barabara ya uhuru,
> Na kuokotwa na mikono ya mtembeaji mwepesi,
> Aliyeelekea bungeni ilikokuwa yake ofisi' (uk.53)

Katika shairi la Kikao cha 'Wanasiasa' (uk.89), mshairi anatueleza jinsi ambavyo wanasiasa wamejiweka tayari kuipora nchi yao. Wanasiasa hao hawana huruma hata kidogo kwa wananchi wanaotaabika.

> 'Hawana jema na jimbi, kwao yote ni hayale.
> Wamenoa visu vyao ili kuichunua ngozi nchi yao' (uk.89).

Kwa mujibu wa gazeti la *The Standard* la tarehe 11 Novemba mwaka wa 2020, Afisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Kuendesha Mashitaka (ODPP) ilifaulu kurejesha ardhi iliyogharimu takribani shilingi bilioni 2.7 iliyokuwa imenyakuliwa. Ardhi hiyo ilimilikiwa na Chuo Kikuu cha Nairobi na nyingine kumilikiwa na shule ya msingi ya Racecourse jijini Nairobi. Jambo hili linadhihirisha mshikamano wa siasa ili kuleta mabadiliko kwa manufaa ya mwananchi.

### 2.1.5 Ukiukaji wa Sheria

Sheria ni mfumo wa kanuni zilizotungwa na bunge au taasisi zilizopewa mamlaka kikatiba kutunga sheria kwa madhumuni ya kudumisha utangamano, utulivu na amani. Kila mwananchi anastahili kutii kwa kufuata sheria bila kujali au kubagua kwa misingi ya kitabaka, wadhifa wa mtu au jinsia. Sheria ambazo zimetungwa zinastahili kulinda kila mwananchi na kuhakikisha kuwa haki zao hazikiukwi. Hali ambapo sheria zimekiukwa, basi vyombo vya dola k.v. mahakama na taasisi zilizopewa mamlaka kikatiba zinastahili kutumia nguvu na kuwaadhibu watu waliozivunja sheria hizo bila mapendeleo. Usalama wa jamii unapodumishwa, bila shaka maendeleo hunawiri.

Katika diwani ya *Kaza Macho*, hali hii ya ukiukaji wa sheria inadhihirika bayana. Katika shairi la 'Niko Hapa' (uk.113), mwandishi anaeleza kuhusu dhiki zilizomkumba mja aliyetiwa mbaroni kwa kosa ambalo hakulitenda. Hali hii inampelekea mja huyu kukata tamaa maishani. Katika kifungu cha pili, mshairi anasema kuwa ametiwa pale jela kwa sababu ya kulaumiwa kwa kupanga njama za kumshambulia mkubwa asiyemfahamu. Katika shairi lilo hilo la Niko Hapa, taswira ya makazi yasiyostahiki imetolewa ambapo wanaohukumiwa na kutiwa kizuizini ni wale ambao hawajafanya kosa lolote na pia wale ambao hawana uwezo wa kujitafutia mawakili ambao wangewapigania. Katika shairi hili, mtunzi ameghadhabishwa na vitendo vya wakubwa na wale walio na nguvu za kiutawala ambao baada ya kutenda kosa la jinai, wao huwawekelea watu wengine tuhuma hizo na kutumia nguvu zao za kiutawala kuhakikisha kuwa wanafungwa. Mfano ufuatao unadhihirisha hali hii:

> "Niko hapa,
> Nikilala sakafuni,
> Penye adha iso kifani,
> Kwa sababu nililaumiwa,
> Kwa kupanga njama,
> Za kumshambulia,
> Mkubwa nisiyemjua ni nani" (kifungu cha pili uk.113).

Katika shairi la 'Kadhia ya Jana' (uk.21), mshairi anasimulia jinsi ambavyo watu wanapigwa kinyama na kuuliwa hadharani.

> Nalikumbuka sana,
> Pigo la kutisha,
> Lililotibua makovu ya juzi,
> Mja alipogeuzwa mzoga…" (kifungu cha pili, uk.21).

Sheria zinapokiukwa, jamii bila shaka hukosa maadili ambayo huwa msingi wa maendeleo. Katika shairi la 'Kadhia ya Jana' (uk.21), mshairi anatueleza jinsi ambavyo wema umegeuzwa kuwa ubaya au uovu. Uzalendo vile vile umekuwa uhaini. Taswira ya jinsi ambavyo binadamu aliteswa kikatili na maungo yake kukeketwa na mtu dhalimu ni dhihirisho tosha kwamba sheria zinakiukwa kila kuchao. Isitoshe, bila huruma yoyote, magenge yalipasua kichwa cha mnyonge huyo. Kwenye shairi la 'Jana na Leo' (uk. 26), sheria inampendelea tajiri na kumkandamiza mnyonge. Licha ya kwamba maskini amejitolea kwa udi na uvumba kulijenga taifa lake,

anakumbana na vizuizi vinavyolemaza juhudi zake. Maskini hao hunyang'anywa mali zao hadharani. Wanapokimbilia mahakamani kupata haki, wenye nguvu hushinda kesi hizo. Kulingana na mshairi, sheria inayotumika ni baguzi, inaegemea upande mmoja na maamuzi ya kesi hizo hufanyika usiku kama inavyodhihirika kupitia mfano ufuatao:

> … "Naikumbuka,
> Sheria iliyokata kumoja,
> Sheria iliyokuwa hatia,
> Sheria iliyohukumu usiku,
> Sheria iliyoamriwa ndotoni,
> Sheria iliyotanda jimboni' (kifungu cha 3 uk.26).

Sheria inapotungwa lengo lake kuu huwa ni kuwahakikishia wanajamii haki zao pasipokuwa na maonevu kwa mja yeyote kinyume na ilivyo katika shairi la 'Nyota ya Huzuni' (uk.40), ambapo mja ametengwa penye haki. Anapokuwa mgonjwa, anakosa kupewa matibabu na badala yake kupuuzwa kama nyani (ubeti wa nne uk.40).

### 2.1.6 Ukoloni

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu, ukoloni ni ule mtindo au mfumo ambapo nchi moja inatawala nchi nyingine. Mataifa mengi katika bara la Afrika yalitawaliwa na nchi zingine hasa kutoka ughaibuni. Madhumuni ya tawala hizo za kikoloni yalikuwa ni kuwabagua na kuwanyonya wenyeji. Taifa la Kenya ni miongoni mwa mataifa hayo yaliyotawaliwa kiimla na wazungu.

Thuranira (2017) akimrejelea Fanon (1963), anasema kwamba mwafrika aliwakilisha maovu machoni pa mkoloni. Hii ina maana kwamba mwafrika huyo alikosa maadili na hivyo basi, iliamriwa kiumbe huyo kudhibitiwa kwa kutumia nguvu kwa madhumuni ya kufanikisha uongozi wa kiimla wa mkoloni. Amri ilitolewa kwa vikosi vya polisi kuwadhibiti raia.

Wananchi walipitia madhila mbalimbali katika kipindi hiki cha ukoloni. Walinyang'anywa ardhi yao iliyokuwa na rutuba na baadhi yao kusalia kuwa maskwota. Sheria iliyokuwepo iliwaruhusu wazungu hao kumiliki ardhi au mashamba katika maeneo yaliyoonekana kuwa na rutuba hivyo kutoa mazao mengi. Waafrika walitumikishwa kwenye mashamba hayo ambapo walifanya kazi kama vibarua. Walitozwa kodi ya kiwango cha juu bila kujali uwezo wao wa kiuchumi. Isitoshe,

watoto wa waafrika hao walipewa elimu duni kwa lengo la kuwafanya kuweza kuajiriwa katika ngazi za chini serikalini. Wenyeji walinyimwa nafasi ya kujiendeleza. Katika kilimo, waafrika hao hawakuruhusiwa kupanda baadhi ya mimea iliyoonekana kuleta hela. Mimea kama vile pareto, chai, kahawa n.k. ilikuwa inapandwa na kukuzwa na wazungu pekee.

Kwenye shairi la 'Uonacho Sicho' (uk.1), mshairi anatueleza kupitia mbinu rejeshi masaibu waliyoyapitia wapiganaji wa uhuru. Waafrika hao waliungana na kushikamana ili kumwaga damu katika kupigania uhuru wao. Baada ya kujinyakulia uhuru, waafrika walikuwa na matumaini ya kuishi maisha mema bila mateso, ndwele au ubaguzi wa aina yeyote.

> "Tukidhani yote, yote yashakuwa ya kale,
> Sasa ni kama ukale,
> Haipo ndwele,
> Uhuru" (kifungu cha tatu uk.1).

Katika tawala za kikoloni, kwenye shairi la 'Jana na Leo' (uk.26), viongozi waliwakataza wananchi kufanya mambo yafuatayo: kuota, kusoma, kusema kwa kudai haki yao. Wananchi walitiwa hofu na hivyo kuwapa nafasi viongozi waliotumikia tawala za kikoloni kuendelea kunyanyasa wananchi. Katika shairi la 'Mkuki kwa Nguruwe' (uk.51), utawala wa wakoloni ulikuwa wa kiimla na uliweza kuwakandamiza wenyeji. Wananchi waliteswa, walidhalilishwa, walifanyishwa kazi, kutozwa kodi ya kuishi na hata walimwaga damu kumaanisha wengine waliuliwa.

> … "Unakumbuka ulivyoteswa na mkoloni?
> Unakumbuka ulivyodhalilishwa na mgeni?
> Ukatumikishwa,
> Ukatozwa kodi ya kuishi,
> Ukatokwa hata na jasho la damu" (ubeti wa uk.51).

### 2.1.7 Ukoloni Mamboleo

Ukoloni mamboleo ni hali ambapo sera za kikoloni zinaendelezwa baada ya taifa kujinyakulia uhuru. Sera hizo zilikuwa kandamizi kwa wananchi. Ukoloni mamboleo unadhihirika kupitia uongozi mbaya. Idadi kubwa ya watu wanateseka ikilinganishwa na ile ambayo inanufaika. Maendeleo katika nchi nyingi ambazo hazina nguvu za kiuchumi yamelemazwa na tatizo hili la ukoloni mamboleo. Masalio ya utawala wa kikoloni yanadhihirika siku hizi kupitia ufisadi,

mafarakano ya mara kwa mara na vita baina ya wenyeji. Idadi kubwa ya viongozi katika bara la Afrika ni washiriki wakuu katika kupalilia na kuendeleza utawala wao.

Baada ya mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni kujinyakulia uhuru wao, wananchi walijawa na matumaini kwamba wangeishi maisha mazuri. Kinaya ni kwamba, pindi tu baada ya kuchukua hatamu za uongozi, viongozi wa kiafrika waliiga mtindo wa kiutawala wa kimabavu. Hao viongozi waafrika walisababisha maafa mapya kwa wananchi wenzao. Katika shairi la '(Uonacho, Sicho uk.1),' mshairi anasema:

> 'Tukidhani yote, yote yashakuwa ya kale,
> Sasa ni kama ukale,
> Tukapiga kelele,
> Haipo ndwele.'

Maneno haya ni ithibati tosha kwamba, uhuru uliopatikana ni wa bendera. Wanaoendelea kufaidika ni viongozi. Wananchi hawana cha kujivunia kamwe. Shida na madhila wanayopitia ni kama zile walizopitia kabla ya kupata uhuru. Katika shairi 'Mkuki kwa Nguruwe…'(uk.51), Viongozi wanaonekana kuwafanyia wenzao madhila. Wananchi hao wanateswa na kuchekwa na hata kudharauliwa.

> … "Kwa nini sema,
> Unawatesa wenzako,
> Unawanyonya watu wako,
> Unawacheka wenye ngozi yako?
> Kwa kuwa leo, umekuwa kiongozi."

Kauli hizi ni thibitisho kuwa baada ya mataifa ya Afrika kujinyakulia uhuru, waliotwikwa jukumu la kuongoza watu waliingiwa na kiburi, tamaa na ubinafsi. Waliwaona wananchi wenzao kama viumbe wasiostahili kutoa sauti ili kuchangia dhidi ya maendeleo yao katika jamii.

### 2.2 Hitimisho

Katika sura ya pili, tumerejelea diwani ya *Kaza Macho* na kuangazia maudhui ya kisiasa yafuatayo: Uongozi wa kiimla, ukiukaji wa haki za kibinadamu, usaliti, ufisadi, ukiukaji wa sheria, ukoloni na ukoloni mamboleo. Katika sura hii, dhana ya siasa imefasiliwa kama mfumo

wa kijamii unaohusu matumizi ya sheria katika kufanya maamuzi ya kiutawala na jamii kama nyenzo ya kuendeleza asasi mbalimbali za kijamii k.v. dini, siasa na uchumi.

Tumebainisha kwamba siasa huwa asasi kuu ya kijamii inayoleta sio tu migongano ya kijamii bali hata mshikamano wa wanajamii. Viongozi walioko wametumia siasa kujitafutia umaarufu badala ya kutatua matatizo yanayowakumba wanajamii. Usaliti umekuwa sehemu ya maisha. Viongozi Waafrika walitarajiwa kuboresha maisha ya wananchi wenzao baada ya mbeberu kuondoka. Badala ya kuwasaidia na kuwaokoa kutoka lindi la ukiwa na ukata, viongozi hao waliwasukumia masaibu zaidi. Waligeuza uzalendo ukawa uhaini na wema ukawa uovu kama inavyodhihirika katika shairi la Kadhia ya Jana (uk.21). Sura inayofuata ya tatu, tumeangazia athari ya siasa kwa jamii.

## SURA YA TATU:

## ATHARI ZA SIASA KWA JAMII

### 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili, tulichambua maudhui ya siasa kama yanavyojitokeza katika diwani, *Kaza Macho.* Sura hii ya tatu, tutaangazia jinsi ambavyo siasa zimeathiri jamii kwa kurejelea diwani iyo hiyo ya *Kaza Macho* katika kutoa mifano ili kuthibitisha maelezo yetu.

### 3.1 Umaskini

Umaskini ni ile hali ya kutokuwa na mahitaji ya kimsingi k.v. chakula, makazi, mavazi, elimu n.k. na humfanya binadamu kuishi maisha ambayo si kamilifu. Masikini mara nyingi hutegemea misaada kutoka kwa wasamaria wema ikiwemo serikali, makanisa, misikiti na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali. Umaskini husababishwa na nchi kukosa sera nzuri kwa wananchi wake hasa sera inayohusu ugavi wa rasilimali za umma. Kulingana na Nyong'o (2001) uongozi bora ndio mkakati faafu kabisa wa kumaliza umasikini katika jamii yoyote. Katika nchi yoyote ambayo inatawaliwa na viongozi ambao wamemakinika katika kutunga sheria ambazo zinaegemea kulinda haki za wananchi wake, suala la umasikini huwa halipo na kama lipo basi huwa kwa kiwango cha chini kabisa. Kila msimu wa uchaguzi unapowadia, wananchi hujitokeza kwa wingi kuwachagua viongozi ambao watawawakilisha katika serikali ili kuhakikisha kuwa mahitaji yao yanapewa kipao mbele. Hata hivyo, baada ya kuchaguliwa viongozi huyaweka masilahi yao mbele na kumsahau mwananchi hadi pale msimu wa uchaguzi unapokaribia tena. Viongozi hawa hupanga sera ambazo zinadhamiria kulinda mahitaji yao ya kibinafsi pamoja na kujilimbikizia rasilimali za umma. Rasilimali wanayobakiza viongozi hao hugawanywa kwa njia isiyokuwa sawa. Wanyonge hukosa sauti na wakati mwingine wanapopiga kura kuwachagua viongozi kwa nia ya kuleta mabadiliko katika maisha yao, viongozi hao huwasaliti kwa kutorokea mijini ambako wamejijengea makasri kuishi maisha ya kifahari.

Taswira ya umaskini inajitokeza katika shairi la 'Tazama' (uk.14). Katika shairi hili, mtunzi amemrejelea maskini kama kiumbe ambacho hakina mahali pa kulala wala chakula cha kutia kinywani. Hawawezi kumudu bei ya chakula ambacho kinazidi kupanda kila kuchao. Maskini hawa wanaendelea kukumbana na mauti kwa sababu ya njaa. Fukara walioko mjini wamesongamana katika mabanda kwenye mitaa duni ambako kuna mirundiko ya taka na tishio la magonjwa hatari. Wengine wao hawawezi kumudu kulipia vyumba hivyo na hivyo kulazimika

kulala barabarani. Wamekosa mavazi bora ya kujisitiri na hivyo kulazimika kuvaa mararu mararu. Fukara hao wanasumbuliwa na maradhi ya aina mbalimbali na baadhi yao hayawezi kutibika. Wanapougua kupata matibabu ni muhali. Gharama za matibabu ni kubwa na maskini hao hawawezi kumudu. Mshairi ameonyesha jinsi masikini wanavyoishi maisha ya kutegemea wahisani kugharamia matibabu na mahitaji yao ya kimsingi. Wakiwa hao wamekuwa watumwa katika makasri ya hao viongozi. Baadhi yao wanalipwa ujira mdogo. Dhuluma wanazopitia maskini hao haziwezi kupigiwa mfano kama inavyodhihirika kupitia mfano huu:

> 'Tazama utaona,
> Maskini wanaoishi katika dhiki za karne,
> Fukara wanaodidimia katika kinamasi cha dhuluma,
> Fakiri wanaogugunwa mili na michonge ya tabaka' (Kifungu cha 1 uk.14).

Vile vile katika kifungu hiki, kilio cha maskini kinajitokeza bayana. Kilio chao ni cha mda mrefu na kimekuwa kikipuuzwa na viongozi ambao wanawadhulumu badala ya kuwasaidia kuyapata mahitaji ya kimsingi. Mapuuza ya viongozi hawa yamesababisha vifo vya wananchi maskini ambavyo vingeepukika iwapo viongozi hao wangewajibika.

Katika shairi la 'Kaza Macho' (uk.17), mtunzi anatuchorea taswira ya banda (nyumba) ambalo liko katika hali duni kabisa. Kibanda hicho kimeinama na kiko karibu kuanguka huku maji ya mvua yakivuja ndani. Katika shairi hili ajuza na shaibu wanachorwa wakiwa wanyonge. Wazee hawa walishiriki katika vita vya kuikomboa nchi yao kwa lengo la kuufukuza umaskini lakini sasa hawana cha kujivunia kamwe. Wamevalia mavazi ambayo yamewasitiri nusu mwili. Ndoto walizokuwa nazo zilizimwa ghafla. Nyuso zao zinaashiria jinsi ambavyo wameteseka kwa kusahaulika na viongozi wa kila awamu kama inavyojitokeza katika shairi la 'Kaza Macho' (uk. 17) ifuatavyo:

> 'Unamwona yule ajuza;
> Mwenye maziwa yaliyoinama kwa ukiwa,
> Mwenye macho mekundu kwa sababu ya moshi,
> Mwenye makunyanzi ya ngozi yanayotisha,
> Mwenye vazi linalomstiri nusu mwili,
> Mwenye mvi mfano wa sembe kichwani,
> Alishiriki harakati za kuikomboa nchi' (kifungu cha 2).

Maisha wanayoishi maskini yamejaa masaibu si haba. Katika shairi la ‘Kiokote’ (uk.34), nafsineni anajisawiri kama mja anayeishi maisha ya kimaskini. Katika kifungu cha nne, anauliza iwapo kuna yoyote anayeweza kumuauni kutoka kwa hali ile ya kimaskini. Vile vile, anatueleza uduni wa makazi yake na jinsi yalivyofurika kuonyesha ni wengi wanaoishi katika hali hiyo ya kimaskini kama inavyodhihirika kupitia mfano ufuatao:

> Ninasakini maskini,
> Yaliyozinga mzingo,
> Madhila ya kudhili,
> Na mateso ya kutesa’ (ubeti wa 1 uk.34).

Uongozi uliopo umewatenga waja hawa kama inavyoelezwa katika shairi la ‘Nyota ya Huzuni’ (uk.40). Maskini wamesahaulika na hivyo kuonekana kukata tamaa. Wameshambuliwa na chawa, funza na kunguni kama inavyoonekana kupitia shairi hilo la ‘Nyota ya Huzuni;

> Ana chawa nyweleni, ona dhiki,
> Na kunguni nguoni, ahiliki,
> Funza na miguuni, wamesaki,
> Ndwele ya kutwishwa!’ (ubeti wa 5).

Katika shairi la ‘Lini’ (uk.36), kupitia masimulizi mshairi anatuchorea taswira ya wanakijiji waliokuwa wakiomboleza hali duni ya maisha wanayoishi. Anamulika kilio cha waja wanaoendelea kulia kwa sababu ya umaskini. Analalamikia mateso wanayopokea kutoka kwa viongozi wao. Wamefutwa kazi kwa madai ya kutozalisha mazao. Wanalipwa malipo duni kwa mazao waliyozalisha wenyewe. Anatamani ije siku ambayo wataomboleza kifo cha dhiki. Kutokana na kuwa na uwezo duni, wanakijiji wanaendelea kuchekwa na ‘Bundi.’ Wanaorejelewa kama ‘Bundi’ ni viongozi katili wanaozidi kuwakandamiza wanyonge kama inavyodhihirika kupitia kifungu kifuatacho:

> ‘Naikumbuka sauti ya mama,
> Alipokuwa akiwinga,
> Bundi aliyekuwa akiimba,
> Mbolezi kuucheka umaskini,
> Kuudhihaki uwezo duni wa wanakijiji’ (kifungu cha 2 uk.36).

Binadamu walioko mijini na mashambani wameathirika pakubwa na umaskini. Viumbe hawa wanalia kutokana na dhiki nyingi ambazo zimewakumba kiasi cha kuwakosesha raha. Wanajamii hawa hawana namna nyingine ya kujipatia kipato ili kuzikimu familia zao. Maisha yamekuwa magumu sana. Kampuni na taasisi za serikali zimelazimika kustaafisha wafanyikazi wake mapema bila kujali jinsi ambavyo jambo hili litaathiri maisha yao. Wanajamii wengi wamekosa ajira kwani wachache waliokuwa nayo wamefutwa na hivyo kukosa hela za kutumia kununua chakula na kulipa karo za watoto wao kama inavyojitokeza kupitia mfano ufuatao, shairi la Mfumo wa Soko Huria (uk.3).

> 'Yanatisha!
> Fedha juu 'meguria, haipendi maskini,
> Chakula chawakimbia, kwamba hawana mapeni,
> Dhiki imewakazia, wanapunguzwa kazini,
> Kama wanayo hatia, ya kumwibia fulani,
> Mfumo wa soko huria' (ubeti wa pili).

Kupitia shairi hili, watoto wa maskini wamenyimwa fursa ya kupata elimu. Kilonzo (2015: 90) akimrejelea Wollstone (1972), anakiri kuwa elimu ni msingi wa vitu vyote maishani na hivyo haipaswi mtu kuikosa. Anaendelea kusema kwamba kutopata elimu ni sawa na kukosa kifaa cha thamani katika maisha. Elimu humfanya mtu kujielewa na vile vile kuielewa jamii yake. Kukosa elimu ni ishara tosha kwamba wanyonge wataendelea kusalia nyuma kielimu na watabaki kuwa gizani. Hawataweza kuzifahamu haki zao. Viwango vya umaskini vinazidi kuongezeka kila wakati kutokana na hili. Mianya ya kitabaka kati ya matajiri na maskini inaendelea kuwa mikubwa. Waliobahatika kusoma vile vile, hawana ajira. Thuranira (2017) anasema kuwa elimu iliyoko Afrika haijakuwa na umuhimu mkubwa kwa jamii nyingi kutokana na sababu kwamba haijasaidia kupunguza viwango vya umaskini. Kwa hivyo, inaonekana maskini wataendelea kunyanyaswa daima na watu ambao wana mali.

Umaskini umekumba taasisi za elimu. Viongozi ambao walichukua uongozi kutoka kwa mkoloni hawakuboresha mifumo ya elimu na miundo misingi yake ili iambatane na mazingira ya bara la Afrika. Shule nyingi nchini Kenya kwa mfano, ziko katika hali mbaya. Hazina miundo msingi ya kutosha inayohitajika. Zimeshuhudia uhaba wa vifaa vinavyotumika kuendeleza elimu. Shule hizo zimekumbwa na uhaba wa fedha ambazo zitatumika kujengea madarasa. Wanafunzi wengi katika shule za aina hii hukumbana na matatizo chungu nzima ikiwemo kunyeshewa na mvua

wakati wa msimu wa mvua, kuathirika na kibaridi na kuvamiwa na miale ya jua wakati wa kiangazi. Aidha, kuna uhaba wa walimu wa kufundisha na wale walioko, wamelemazwa na mzigo mkubwa. Madarasa yaliyoko hayatoshei kumudu idadi kubwa ya ongezeko la wanafunzi katika shule za umma. Kwa hivyo, kumeshuhudiwa msongamano mkubwa wa wanafunzi hao darasani. Ili kukata kiu ya elimu, wanafunzi hao hulazimika kusomea chini ya miti ambako wanaandika kwenye mchanga kama inavyodhihirika kupitia shairi la 'Chini ya Mgunga' kifungu cha 1 uk.53.

Kupitia shairi la 'Kumekucha' (uk.90), mshairi anatueleza kwamba vijana wa kuranda randa mitaani almaarufu chokoraa, wamechoka kulala barabarani mahali ambapo kuna uchafu mwingi. Vijana hao wamekosa mavazi ya kujisitiri, wamekosa viatu na chakula cha kutia tumboni. Chokoraa hao wanatoa lalama kwamba wakati mwafaka umefika ili kukombolewa kutoka kwa dhiki hiyo ya umasikini inayowakumba kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao:

> 'Kumekucha!
> Kulala barabarani, na uchafu wa njiani,
> Bila kivazi mwilini, au vyatu miguuni,
> Wala mlo kitumboni, au kinywaji kinywani,
> Nitolewe matopeni, penye mateso ya zani,
> Kumekucha kulichele!' ubeti wa 6.

Ugumu wa maisha miongoni mwa familia nyingi katika jamii umepelekea wasichana wa umri mdogo kuozwa na wazazi wao ili kupunguza mzigo wa mahitaji k.v. chakula na karo. Mahari, ardhi, fedha kidogo na ahadi kwamba mume ataenda kugharamia mahitaji ya msichana hutolewa. Hatimaye msichana hukabidhiwa mume wake kuandamana naye kwenda kutekeleza majukumu ya nyumbani ya huyo bwana na pia kushiriki katika shughuli za kilimo. Gazeti la *The Standard,* tarehe 15 mwezi wa Desemba mwaka wa 2020, liliripoti visa vya wasichana chini ya umri wa miaka 18 kuozwa kwa sababu ya umaskini uliozifanya familia nyingi kushindwa kumudu gharama ya chakula nyumbani na malipo ya karo shuleni. Shirika la Muungano wa Mataifa Ulimwenguni (U.N.), lilinukuliwa kuripoti kwamba takribani nusu milioni ya wasichana chini ya umri mdogo wa miaka 18 wanaofiwa kuolewa ulimwenguni. Idadi kubwa ya wasichana hao ikiwa ni kutoka bara la Afrika na Asia. Katika kisa kimoja k.m. huko Uttar Pradesh India, msichana wa miaka 13 aliwajulisha maafisa wa usalama kwamba babake mzazi ambaye hajaajiliwa alinuia kumwoza bila idhini yake. Mahari ya shilingi za Kenya 75,857 au 50,000

ambazo ni rupia za India zilikuwa tayari zimetolewa. Askari walifaulu kutibua njama hii na mzazi wake kutiwa mbaroni.

Gazeti la *The Standard*, tarehe 15 Desemba, 2020 liliarifu kuwa huko Bangladeshi, kulifanyika njama ya msichana mmoja kuolewa akiwa na umri mdogo. Familia ilijitetea kwa kutoa madai kwamba haikuwa na uwezo wa kiuchumi na hivyo ugumu wa maisha uliwasukuma kupanga ndoa hiyo. Vyombo vya dola vilishauri familia kuhusu athari za ndoa za mapema kwa msichana wao. Miongoni mwa athari hizo ni msichana kukatiza masomo yake na uwezekano wa kushika mimba kabla yeye kuwa tayari huwa mkubwa. Wazazi hao waliahidi vyombo vya usalama kutomwoza kabla hajatimiza umri au kuwa mtu mzima. Ajabu ni kuwa baada ya maafisa hao kuondoka, ndoa hiyo ilifanyika saa nane usiku. Jambo la kuhuzunisha ni kuwa kumeshuhudiwa ongezeko la ndoa za watoto katika kambi za wakimbizi tangu mlipuko wa janga la Korona uliozifanya familia nyingi kulemewa na Maisha. Baadhi ya wasichana hupinga na kukataa njama hii ya kuozwa na wazazi wao wangali shuleni. Wasichana hawa wametamani kukata kiu ya elimu kama inavyojitokeza kupitia shairi la ‘Kumekucha’ kifungu cha 2 uk.90.

Katika shairi la ‘Kipofu na Kichaa’ (uk.78), wananchi wanalalama kwa sababu ya umaskini. Wananchi walijitayarisha wakapiga kura kumchagua kiongozi wao wakiwa na matumaini kwamba kiongozi huyo atapambana na kuwanusuru kutoka kwa dimbwi hili la umaskini. Uchaguzi ulipokamilika, wapiga kura waliendelea kummiminia kiongozi wao mpya sifa kem kem wakiwa na lengo la kubadilishiwa mfumo wa maisha yao. Nyimbo zilitungwa kutekeleza jambo hilo kama inavyoonekana kupitia kifungu kifuatacho:

> ‘Akakaa kigodani, tukarudi majumbani,
> Bado twaimba vinywani, tukimsifu fanani,
> Kuwa na umaskini, ulotuvaa mwilini,
> Tautia kiganjani, aubinginyie ndani,
> Utoweke kijijini, nasi tuwe furahani…’ (kifungu cha 3).

Mfano huu unaashiria kwamba wananchi hawana cha kujivunia na wanatamani sana ifike siku ambayo kiongozi wao mpya atafaulu kupambana na umaskini uliosababishwa na viongozi katili waliofilisisha jamii kwa kuipora rasilimali yake k.v. migodi na madini mengineyo (uk.79).

## 3.2 Tamaa na Unyanyasaji

Tamaa ambayo inadhihirika katika diwani, *Kaza Macho* ni tamaa ya mali na ya uongozi au utawala. Tamaa inayohusu ongezeko la utawala iliwapelekea wazungu kutwaa mataifa ya bara la Afrika na kuyaweka chini ya himaya yao. Tamaa hii iliwafanya wakoloni kuwatesa na kuwadhalilisha wenyeji kwa njia mbalimbali. Walitozwa kodi ya juu ya kuishi, walifanywa vibarua vya kutumikishwa na kulimishwa katika mashamba waliyonyanganywa kama inavyojitokeza kwenye shairi la 'Mkuki kwa Nguruwe' (uk.51). Kwa sababu ya uongozi, waliochukua mamlaka kutoka kwa mkoloni, wanazidi kuwakandamiza wananchi kwa madhumuni ya kuwanyamazisha ili waendelee kuitawala nchi. Viongozi hao wameingiwa na kiburi kinachowafanya kucheka na kuwadharau waafrika wenzao. Bila huruma, watawaliwa wanateswa na kuzidi kunyonywa damu kama inavyodhihirika kupitia shairi hilo la 'Mkuki kwa Nguruwe' (kifungu cha 3 uk.51). Tamaa imewafanya wanasiasa kukatalia uongozini, hawataki kubanduka. Wananchi wameonekana kushindwa kuwang'oa mamlakani. Viongozi hao wanaamini kuwa mamlaka waliyo nayo ni urithi kutoka kwa mababu zao hivyo, kuwaondoa mamlakani ni sawa na kuvunja mwiko kama inavyojitokeza katika kifungu kifuatacho katika shairi la 'Kibuyu' (uk.58):

> Tutafanya jambo gani?
> Hii hali tuliyoko, yatuwangisha vichwani,
> Kibuyu nyoka aliko, ni urithi wa zamani,
> Tuloambiwa ni mwiko, tusikivunje katani,
> Nyoka yumo kibuyuni,
> Tutafanya jambo gani? Ubeti wa 4.

Tamaa ya mali kwa viongozi inajitokeza katika shairi la 'Adha Yetu' (uk.60). Baada ya viongozi kupata idhini ya kuongoza jamii, huingiwa na ulafi au uroho. Wanabuni mbinu ya kuchimbua na kuwaibia utajiri na hazina zote za jamii. Kwa mujibu wa gazeti la *The Standard* la tarehe 11 Novemba mwaka wa 2020, Afisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Kuendesha Mashitaka (ODPP) ilifaulu kurejesha ardhi iliyogharimu takribani shilingi bilioni 2.7 iliyokuwa imenyakuliwa kutokana na viongozi kuwa na tamaa ya kupata mali. Ardhi hiyo ilikuwa mali ya Chuo Kikuu cha Nairobi na nyingine kuwa miliki ya shule ya msingi ya Racecourse jijini Nairobi. Viongozi waliopewa majukumu ya kulinda rasilimali za umma wanakosa utu wanapoanza kuwatapeli wananchi kama inavyojitokeza katika ubeti ufuatao:

> Adha ya kutisha ya mataifa yetu,

Ni viongozi wenye tamaa ya vitu,

Wanaotapeli na kuwadhili watu,

Huku wakisema 'Hii ni mali yetu' ubeti wa 3.

Katika shairi la 'Kipofu na Kichaa' (uk.78), tamaa ya kupata mali ilisababisha kiongozi aliyechaguliwa kupora madini na rasilimali ya jamii na hivyo kuwaacha wanajamii wakisononeka na kugubikwa na lindi la umaskini, (uk.84). Kwa sababu ya tamaa ya kupata mali, viongozi wanawanyang'anya waja mali zao hadharani kama inavyodhihirika katika shairi la 'Utenzi wa Ndovu na Mja' (uk. 104-109). Kwenye shairi hilo, Ndovu wanaowakilisha viongozi wenye nguvu za kiuchumi, wameapa kunyonya wanyonge damu yao.

'Ndovu hapo kachemua,

Pumzi kazipumua,

Kwa jua wala mvua,

Hapa nitakwamiliya' ubeti wa 48. `

Wewe mja la kufanya,

Ni miti kuikusanya,

Boriti, mitamba panya,

Nyingine kujijengeya' (ubeti wa 49).

Katika shairi la 'Kivuli' (uk.5), mtunzi analalamika kuwa mtu ananyang'anywa kile alichonacho, alichokitegemea kisha anahitajika kuomba kitu kile kile. Katika shairi la 'Kaza Macho' (uk.17), ajuza na shaibu wananyanyaswa kwani baada ya kupigania ukombozi, wanaachwa katika umaskini bila kufurahia matunda. Kisha matunda ya jasho lao yanaishia kuliwa na wengine. Katika shairi la 'Ulifanya nini' (uk.18), mtu aliyeshinda uchaguzi kwa kupigiwa kura nyingi ananyang'anywa ushindi huo. Anaambiwa hana akili kwa kile alichokijua na analazimishwa kusema mambo ambayo hakufanya ili kujinusuru.

### 3.3 Utabaka

Utabaka ni hali ambapo watu wana ngazi tofauti za kijamii. Kuna wale wa ngazi za juu, ngazi ya wastani na ngazi ya chini. Katika baadhi ya mashairi, watunzi wamesawiri jamii kuwa imegawika katika matabaka mawili makuu; tabaka la juu na lile la chini. Tabaka la juu linahusisha walala hai na lile la chini likihusisha walala hoi. Viongozi na vibaraka wao hujumlishwa katika tabaka la juu huku wananchi wakiwa katika tabaka la chini. Idadi ya walala

hai huwa ndogo inapolinganishwa na walala hoi ambao huwa wengi katika jamii. Taswira ya maisha ya tabaka la juu yanaashiria kwamba hawaishi maisha ya dhiki kinyume na ilivyo kwa tabaka la chini. Tabaka la juu linaishi kwenye mitaa ya kifahari na kula vyakula vitamu ambavyo vimefanya vitambi na shingo zao kunenepa. Wanapougua, wana uwezo wa kupata tiba bora.

Katika diwani ya *Kaza Macho,* utabaka unajitokeza kupitia mashairi yafuatayo; Kwenye shairi la ‘Mfumo wa Soko Huria’ (uk.3), matajiri hao wana pesa nyingi zilizo mifukoni na benkini. Pesa hizo wamezipata kupitia wizi wa mali ya viwanda kama inavyojitokeza kwenye kifungu kifuatacho.

> Yaumiza;
> Walojilimbikizia, pesa nyingi mifukoni,
> Hata walojiibia, hivi hivi hadharani,
> Tija wanatarajia, wacheka hadi benkini,
> Ila fukara sikia, walia hadi nyumbani,
> Mfumo wa soko huria!

Katika shairi la ‘Kiokote’ (uk.34) nafsi neni anaeleza kuwa ameingizwa kwenye lindi la umaskini na watu wa nasaba bora, yaani wenye mali. Katika shairi la ‘Tazama’ (uk.14), kuna maskini wanaoteseka kwa madhila wanayopitia ikiwemo kukosa mambo muhimu ya kimsingi kama vile chakula (kifungu cha 1). Kwa upande mwingine kuna walio na chakula kwa wingi hadi kushiba wakanenepa kama kiboko, kifungu cha pili. Hivyo masikini wapo katika tabaka la chini na walioshiba na kunenepa ni wale wa tabaka la juu.

Pia katika shairi la ‘Uhuru’ (uk.15), maendeleo yamebakia kwa wenye vitambi yaani walio na mali. Kwa viongozi hawa ambao wanapora mali ya umma, sera imekuwa ni ngome yao. Dini inapendekezewa walio katika shida kama inavyojitokeza kupitia mfano ufuatao:

‘Dini imekuwa liwazo la wadidimiao katika dhiki’… kifungu cha 4. Katika shairi la ‘Lini’ (uk. 36), wanyonge wanadhulumiwa na watu wa tabaka la juu. Kwa mfano, katika kifungu cha 3 ndugu analalamika kwa kutolipwa fidia baada ya kukatwa kidole na mashine ya kutengeneza karatasi. Vile vile mkulima katika kifungu cha 4 analalamikia kutofaidika kwa kuzalisha mazao ambayo faida yake inamwendea mtu mwingine. Shairi la ‘Kaza Macho’ (uk.17), kuna tabaka la chini la akina ajuza na shaibu. Lile banda lenye hali duni ni tabaka la chini. Kwa upande wa pili, matajiri wanamiliki majengo makubwa katika mitaa ya kifahari. Wamefuga majibwa yaliyo na

afya nzuri ya kuwawekea usalama kwa sababu ya kuwa na hela nyingi ambazo wanahesabu kwa kutumia mashine ndogo. Sampuli hii ya watu ndio mshairi anaeleza kuwa wao ndio hufurahia matunda ya uhuru.

Katika shairi la 'Mgonjwa,' matajiri hawa huchukua mali ya maskini kwa nguvu na kuwalazimisha kuhama makwao kama inavyojitokeza hapa chini;

> 'Nimewaona wana wake,
> Wakinyongwa kiholela,
> Wakiteswa kihayawani,
> Wakilazimishwa kuhama,
> Wakimwacha mzazi wao macheleni akiugua' (ubeti wa 4 uk.19).

Katika shairi la 'Mwanga' (uk.24), viongozi matajiri wa tabaka la juu wameketi kwenye vivuli huku wakiucheka ujinga. Viongozi hawa hawana shida ya njaa. Wanasherehekea maendeleo yasiyoonekana.

### 3.4 Vita na Tanzia

Vita vya ukombozi kutoka kwa mkoloni vilisababisha umwagikaji wa damu. Waafrika walipochokeshwa na dhuluma kutoka kwa mkoloni, walishiriki vita ili kupigania ukombozi wao. Viongozi waanzilishi kama vile Jomo Kenyatta kutoka Kenya, Julius Nyerere wa Tanzania, Kenneth Kaunda kutoka Zambia, Samora Machel wa Mozambique, Kwame Nkrumah wa Ghana, Robert Mugabe kutoka Zimbambwe na Nelson Mandela kutoka Afrika Kusini, walioongoza vita hivyo vya uhuru. Viongozi hawa walishirikiana na wazalendo wengine kupigania ukombozi katika nchi zao. Mauaji ya wazalendo hao yalifaulu kuzikomboa nchi dhidi ya minyororo ya mbeberu kama inavyodhihirika katika shairi la Mkuki kwa Nguruwe:

> 'Lakini hatimaye,
> Lipochukia kunyanyaswa,
> Lipambana na mateso,
> Kukuru kakara, kukuru kakara, kukuru kakara,
> Hatimaye akaubwaga ukoloni pwaa!
> Ikawa enzi mpya' (kifungu cha 2, uk.51).

Ajabu ni kuwa baadhi ya viongozi waanzilishi kama vile Robert Mugabe miongoni mwa wengine, waliishia kuwa vizuizi vya ukombozi kikamilifu. Nchini Uganda, kwa mfano, kuliripotiwa visa vya mauaji ya halaiki yaliyotokea baada ya kiongozi wa upinzani, Robert Kyagulanyi almaarufu 'Bobi Wine,' kutiwa mbaroni. Kwa mujibu wa gazeti la *The Daily Nation* la tarehe 23 Novemba 2020, takriban watu arubaini walipoteza maisha yao huku mamia wakiachwa na majeraha. Picha na video zilizotumwa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha watu kadhaa wakiwa wamelala katika barabara za jiji wakiwa wamefuja damu nyingi ajabu. Inadaiwa walipigwa risasi na vyombo vya kiusalama. Waliomuunga mkono 'Bobi wine, walimwona kama kijana anayefahamu changamoto zao na kuweza kuzitatua.

Viongozi walioko katika bara la Afrika wamekatalia uongozini. Wamebadilisha katiba za nchi zao ili kuwaruhusu kuendelea kutawala. Raisi wa sasa wa Uganda, bwana Yoweri Kaguta Mseveni kwa mfano, ameongoza nchi hiyo kwa miaka 34. Amebadilisha katiba ya nchi hiyo mara mbili ili kumwezesha kuwania uchaguzi wa mwaka wa 2021 kwa awamu ya sita. Maraisi wengine ambao wamebadilisha katiba za nchi zao ili kuendelea kusalia afisini ni raisi wa Rwanda, bwana Paul Kagame. Vita vilizuka katika nchi ya Cote d'Ivoire baada ya raisi wa nchi hiyo bwana Alassane Quattara kuamua kusalia afisini baada ya mda wake kukamilika. Nchini Kenya, kuna shinikizo la kubadilisha katiba kwa mara nyingine baada ya katiba hiyo kupitishwa mnamo Agosti mwaka wa 2010. Baadhi ya wanasiasa walioko katika serikali wamekuwa katika mstari wa mbele kupigia debe katiba hiyo. Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani, mheshimiwa Raila Odinga, wamekuwa wakiongoza wakenya kutetea kielelezo hicho cha katiba. Juhudi hizo zimepata pingamizi hasa kutoka kwa naibu wa raisi, mheshimiwa Wiliam Samoe Ruto na viongozi wanaomuunga mkono. Wanaounga mkono kielelezo cha katiba, wameamini kwamba katiba hiyo ndiyo itakayokuwa suluhu dhidi ya machafuko au vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyotokea kila msimu wa uchaguzi.

Kupitia shairi la 'Jumamosi' (uk.123), mshairi anatoa taswira ya mauaji yaliyofanyika ya wananchi wasiokuwa na hatia. Majambazi waliokuwa na nia ya kuvuruga uzalendo wa nchi waliwaua bila kubagua kwa misingi ya jinsia, hali au umri. Wote walifagiliwa bila huruma tena mchana peupe.

> 'Ikawa ni patashika, roho tunazitapia,
>
> Watu wakahamanika, wapi pa kukimbilia,

Na bunduki zaalika, kaini wafyatulia,
Ikawa kusalimika, ni satua ya jalia,
Wakatuvamia,
Waua bila huruma, si mzazi si mtoto'… (kifungu cha 2).

Nchini Kenya, mauaji kama hayo yalitekelezwa. Majambazi walivamia jumba la Westgate Mall na kuwaua watu wasiokuwa na hatia. Baada ya uvamizi huo, serikali iliwajibika kwa kuwatuma wanajeshi wake kwenye jengo hilo ambako walidhihirisha ubabe wao kuwasaka wahalifu hao na kufaulu kuwaua wote kama inavyodhihirika kupitia mfano ufuatao:

'Wakasakwa madarini, na kote kule jengoni,
Guruneti mkononi, zisiwafae mwishoni,
Bunduki za mikononi, zikasinyaa milini,
Wakaangushwa chini, wakaramba sakafuni
Wakatuvamia;
Kile cha mtema kuni, wakakijua ni nini,
Ukesha wao uneni, na majigambo ya nyani,
Tukapumua nyoyoni, hata rais ikuluni,
Wakaona mwali, mwali, mwali! (kifungu cha 7 uk.125).

**3.5 Viongozi Kung'atuliwa Mamlakani.**

Wananchi wamechoka na tabia za wanasiasa wao kuwaongoza kiimla. Wamekataa kata kata kuendelea kunyanyaswa. Katika shairi la 'Anguko la Jibwa' (uk.43), wananchi waliokuwa na ghadhabu walimng'atua kiongozi wao mamlakani na uongozi wake ukafikia ukingoni. Licha ya kuwa kiongozi huyo alikuwa na ujasiri, sasa amesalia katika mateso.

Katika shairi la 'Ndege wako Mashakani' (uk.45), mshairi anaonyesha uwezo walio nao watawaliwa kuwaondoa viongozi wasiostahili mamlakani. Anataja jinsi viongozi mbalimbali watakavyoangamizwa kwa manati na panda. Hili linaonyesha kwamba viongozi na hila zao watang'atuliwa mamlakani. Hali hii ilidhihirika nchini Zimbambwe wakati raisi Robert Mugabe alipong'atuliwa mamlakani na jeshi la nchi hiyo baada ya kuongoza taifa hilo kwa miaka mingi. Wananchi wanaonekana kuchokeshwa na viongozi wao walaghai ambao wamekaa uongozini kwa miaka mingi bila kufanya maendeleo yoyote. Wapiga kura sasa wamezinduka na wameamua kuwaondoa mamlakani kwa kutowapigia kura.

### 3.6 Utamaushi

Utamaushi ni hali ya mtu kukata tamaa na kukosa matumaini. Suala la utamaushi hutokana na dhiki zinazowakumba wanajamii kiasi cha kukata tamaa ya kuendelea kuishi. Dhiki hizi mara nyingi husababishwa na uongozi dhalimu unaowakandamiza na kuwanyanyasa wananchi wake. Katika diwani *Kaza Macho,* swala hili limedhihirika katika mashairi yafuatayo:

Kwenye shairi la 'Uliambiwa' (uk.126), mshairi anasawiri taswira ya mja mwenye majuto anayeelekea kukata tamaa kwa kupuuza au kutotenda alichoambiwa mapema. Kila kifungu cha shairi hili kinazungumzia suala fulani linalopelekea mhusika kukata tamaa kwani anajuta kwa kutotenda aliyoambiwa. Kwa mfano, kifungu cha kwanza kinazungumzia suala la elimu. Mhusika aliambiwa asome kwa bidii lakini sasa analia. Kifungu cha pili kinazungumzia suala la uzembe. Mhusika alionywa kuhusu uzembe akapuuza.

Katika shairi la 'Niko Hapa' (uk.113), mwandishi anaeleza kuhusu dhiki zilizomkumba mja aliyetiwa mbaroni kwa kosa ambalo hakulitenda. Hali hii ya ukosefu wa haki katika jamii inampelekea mja huyu kukata tamaa maishani.

Shairi la 'Mpanda Ngazi na Washika Ngazi' (uk.95), tunawaona washika ngazi wanaelekea kukata tamaa baada ya kiongozi wao kujitenga nao na hata kuwadharau (ubeti wa 11). Wanakata tamaa ya ahadi walizoahidiwa na kiongozi wao.

### 3.7 Hitimisho

Tumetamatisha sura ya tatu kwa kuangazia athari za siasa katika jamii. Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na: umaskini, tamaa na unyanyasaji, utabaka, vita na tanzia na viongozi kung'atuliwa mamlakani. Sura itakayofuata, tutashughulikia mbinu za kisanaa zilizotumiwa kuendeleza maudhui ya kisiasa katika diwani *Kaza Macho.*

# SURA YA NNE:

# MBINU ZA KISANAA

## 4.0 Utangulizi

Ili kuafikia mojawapo ya malengo yetu ya utafiti, tumebainisha mbinu za kisanaa ambazo zimetumiwa na mwandishi ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui yake. Mbinu za kisanaa hurejelea matumizi ya vifungu vya maneno kwa ubunifu mkubwa kwa nia ya kuifanya lugha iwe ya kuvutia ili kuufanya ujumbe kueleweka zaidi. Katika utafiti wetu, tumejifunga kwenye matumizi ya lugha na tamathali za usemi. Kupitia matumizi ya lugha, maudhui huwasilishwa na kuwafikia wasomaji wake. Wamitila (2008) anaeleza kuwa tamathali hizi za usemi zinakuwa na mchango mkubwa sana katika fasihi. Zinafanya kazi ya fasihi sio kuwa yenye mvuto au kuwa na msisitizo tu bali kuifanya iwe ya mnato mkubwa. Katika diwani hii ya *Kaza Macho*, mtunzi wa mashairi haya amedhihirisha kubobea kwake kwa kutumia tamathali mbalimbali za usemi. Mifano ya tamathali zilizoshamiri katika diwani hii ni pamoja na:

## 4.1 Tamathali za Usemi.

### 4.1.1 Jazanda

Jazanda ni mbinu inayofananisha vitu viwili au zaidi kwa mafumbo. Ni mbinu ambapo mwandishi hutumia lugha fiche au lugha ya kimafumbo kuwasilisha ujumbe wake. Humhitaji mlengwa au msomaji kufikiria kwa undani ili kuweza kung'amua maana iliyokusudiwa pasi kubadilisha maana lengwa k.v. 'kigogo' kurejelea kiongozi mwenye mamlaka ya kiutawala na ya kiuchumi. Katika ngojera ya 'Mpanda Ngazi na Washika ngazi' (uk.95), 'Washika ngazi' ni jazanda ya wanyonge, maskini ambao walimsaidia kiongozi wao ambaye ni mpanda ngazi kupata madaraka kwa kumpigia kura.

Katika shairi la 'Jogoo' (uk.42), neno 'jogoo' limetumika kuwarejelea viongozi ambao wako mamlakani na wamejawa na tamaa na ubinafsi. Viongozi hao wanatawala kwa kuwatesa wanyonge. Vigogo hawa wanawaona wanyonge kuwa mbumbumbu na hawajawazia hata siku moja kuwa wananchi wanaweza kuzinduka na kuwaondoa madarakani. Mshairi anaeleza kuwa uongozi wa kigogo huyo utafika mwisho na maovu yote kuwekwa wazi. Mateso yakidhihirika wananchi watakuwa wenye furaha ya kujikomboa (ubeti wa 3).

Katika shairi la ‘Anguko la Jibwa’ (uk.43), ‘jibwa’ limetumika kwa maana ya kiongozi anayetawala kwa ushujaa pasipo kuwajali wananchi wake. Jazanda hii imetumika kuwatahadharisha viongozi wanaochukua mamlaka dhidi ya kuwatesa watawaliwa kuwa siku moja watanga’tuliwa mamlakani.

Katika shairi la ‘Ndege wako Mashakani’ (uk.45), mwandishi ametumia jazanda ya ndege kwa maana ya viongozi. Anaelezea uwezo walio nao binadamu katika kuwaondoa viongozi hao mamlakani. Anataja jinsi ndege (viongozi) mbalimbali watakavyoangamizwa kwa manati na panda. Hili linaashiria kwamba viongozi hao katili wataondolewa mamlakani.

Mshororo wa tatu katika ubeti wa nne wa shairi ‘Uonacho Sicho’ (uk.1), mwandishi ametumia maneno ‘sauti ya fisi’ kumaanisha watu ambao wamejawa na tamaa kupindukia. Katika shairi la Ijumaa, kuna matumizi ya jazanda ambapo mwandishi anasema kuwa, ‘Mbali huko nilisikia cheko la fisi…’ ‘Fisi’ ni mnyama ambaye kwa kawaida anahusishwa na tamaa na ulafi. Sifa hizi zinamfanya fisi huyo kuwa na ubinafsi wa kujitakia yeye mwenyewe bila kuwajali wenzake. Neno ‘fisi’ katika muktadha huu limetumika kuwarejelea wanasiasa tapeli wasio na utu wowote na wenye tamaa.

Katika shairi la ‘Kikao cha Wanasiasa’ (uk.89), jazanda inajitokeza katika ubeti wa mwisho ambapo tunajulishwa kuwa wanasiasa ndio majimbi. Neno ‘majimbi’ lina maana ya vigogo au viongozi ambao wana mamlaka ya ajabu. Mshairi anasema pia kuwa kuichuna ngozi nchi yao kumaanisha kujilimbikizia mali ya umma. Mbinu hii ya jazanda ina umuhimu mkubwa sana kwa msomaji. Inamsaidia kukuza uwezo wake wa kufikiria na uwezo wa kudadisi.

### 4.1.2 Tashbihi

Hii ni mbinu ya kulinganisha kitu na kingine kwa kutumia viungio: fanana na, kama, minghairi ya, sawa na, mfano wa, tamthili ya na ja. Ulinganishi huu kwa kawaida unakusudiwa kusisitiza sifa maalumu kwa kujenga picha ya kitu au hali fulani akilini. Katika shairi la ‘Nyota ya Huzuni’ (uk.40), ubeti wa 4 mwandishi anasema, ‘Kwa tiba apuuzwa kama nyani.’ Hapa mtunzi anasisitiza jinsi tabaka la wanyonge linavyodhalilishwa kwa kunyimwa matibabu.

Katika shairi la ‘Pendo’ (uk.41), mshairi anasema ‘…hilo msiandame, lahasiri kama kondo.’Pendo ambapo mja hampendi mwenzake ndilo mshairi anaelezea kuwa linaangamiza kama vita. Anasisitiza umuhimu wa umoja na usawa katika jamii na kwamba watu waweze

kuwathamini wenzao. Katika shairi la Mkuki kwa Nguruwe (uk.51) kifungu cha pili, mwandishi anasema, '…Ukasema shida zimeruka kama ndege,' kusisitiza jinsi mwafrika alivyojikomboa kutoka kwa mkoloni na kudhania kuwa shida zitamalizika.

Katika shairi la 'Ina Nini' (uk.71), mtunzi analinganisha tabia ya waja waliojitosa siasani ya kutusiana hadharani na tabia za kuku. 'Kwa nini, watusiane njiani, hata tusi za nguoni, ja kuku wakirukia, na kwa nyundo, kujitosa siasani?' ubeti wa saba mshororo wa 2. Kwa kawaida kuku huwa na tabia ya kudona donana wenyewe huku wakichakura chakura wakitafuta chakula. Wanapopigana, hutoana manyoya na hivyo kusababisha kutokea kwa majeraha katika miili yao. Wanasiasa wanafananishwa na tabia ya kuku wanaposhiriki katika ugomvi wa hadharani kwa matusi yanayokusudia kuharibiana sifa. Tashbihi hii imetumika kuwatahadharisha wanasiasa kukoma kuchafuliana sifa mbele ya wapiga kura bila kuwa na aya. Badala yake ushindani wa kisiasa uwe ni wa kisera na wala sio matusi.

Katika shairi la 'Kipofu na Kichaa' (uk.78) ubeti wa mwisho, wanakijiji wanasema kuwa kiongozi waliomchagua aliwaona 'wajinga kama nyani,' kwani baada ya kumchagua anatumia mamlaka yake kuwaibia mali yao.

Kwenye shairi la 'Uonacho Sicho' (uk.1), katika ubeti wa tatu mshororo wa pili, mshairi anaeleza kwamba sasa ni 'kama' ukale, kuashiria kwamba hali haijabadilika. Wanyonge wanadhulumiwa jinsi ilivyokuwa zamani. Katika shairi la 'Nungubandia' (uk.55), ubeti wa pili mshororo wa pili, kuna matumizi ya mbinu hii ambapo matendo ya mwanasiasa yanalinganishwa na mnyama. Mshairi anasema kuwa 'mwanasiasa, kichwa chake mithili ya kiboko akitingisha.' Mbali na kuleta ulinganisho ambapo kitu kimoja kinalinganishwa na kingine, kwa kiwango kikubwa tashbihi husaidia kuchimuza toni ya shairi. Tashbihi hizi zimetumika kuchimuza maudhui yanayorejelewa katika ushairi na kazi nzima ya kisanaa.

### 4.1.3 Tabaini

Tabaini ni mbinu ambayo hutumia silabi 'si' katika kusisitiza ujumbe wake. Kusisitiza huku hujitokeza kwa njia ya kinyume. Katika shairi la 'Kipofu na Kichaa' (uk.78), mtunzi anasisitiza jinsi ambavyo kiongozi aliyechaguliwa na wanakijiji na baadaye kuwasaliti alisifika kote kijijini. Katika kifungu cha pili, mtunzi anasema, 'si mijini si njiani, wote wataja fulani.' Katika shairi hilo hilo katika kifungu cha kwanza, mshairi anasema 'si cha sasa cha zamani, ila kingali

kichwani,' kurejelea kisa. Tamathali hii imetumika kusisitiza umuhimu wa kisa anachosimulia kuhusu kiongozi na kwamba waja waweze kuweka makini yao kwenye masimulizi na hatimaye wafanye uamuzi unaofaa.

Kuna matumizi ya mbinu hii katika shairi la 'Jumamosi' (uk.123). akirejelea matendo ya majambazi waliovamia watu katika jengo, mshairi anasema, …si kutenda si kunena' kifungu cha kwanza. Katika kifungu cha pili cha shairi hilo, mshairi anasema kuwa majambazi hao waliwaua watu bila kubagua: 'Waua bila huruma, si mzazi si mtoto,' (uk.123) kuonyesha na kukemea ukatili wa hao magaidi.

### 4.1.4 Tanakali za Sauti

Hii ni mbinu ambapo mwandishi hutumia maneno fulani ili kuiga mlio wa hali fulani. Mbinu hii ya sanaa vile vile huitwa onomatopoeia. Maneno ambayo yanatumiwa huonyesha namna sauti inayorejelewa inavyosikika. Katika shairi la 'Ijumaa' (uk.56), kuna matumizi ya tanakali za sauti. Ili kusisitiza ujumbe wake kuhusiana na swala la ugaidi, mshairi anajenga picha au taswira kwa kutumia tanakali za sauti kama inavyodhihirika hapa: 'Vigae vilivyopeperushwa peperu…' (kifungu cha 1) kuashiria uharibifu mkubwa wa majengo na mali ya watu na ya umma.

Kuna matumizi ya tanakali za sauti katika shairi la 'Mkuki kwa Nguruwe' (uk.51) ubeti wa pili mshororo wa nne ambapo mwandishi anaelezea juhudi walizoweka katika kupambana na mkoloni aliyekuwa akiwakandamiza kwa siku nyingi. Anadokeza kuwa wazalendo walipambana na hayo mateso 'kukuru kakara, kukuru kakara, kukuru kakara' (uk.51). Katika shairi hilo la Mkuki kwa Nguruwe, mwandishi pia anasema, '…hatimaye ukaubwaga ukoloni chini pwaa!' kusisitiza kujikomboa kwa mwafrika kutoka kwa mkoloni. Tanakali hizi zimetumika ili kusisitiza ujumbe unaowasilishwa na mshairi.

### 4..1.5 Maswali ya Balagha

Huwa ni maswali ambayo wakati mwingi hayahitaji majibu ya moja kwa moja kwa kuwa majibu yake yanafahamika wazi. Maswali ya balagha hutumiwa kudadisi ili kueleza jambo fulani kwa kina. Vile vile, hutumiwa kuzindua hasa wasomaji wa ushairi. Maswali haya yanatumika kuchochea fikra za msomaji au hadhira, kutoa hisia za ndani na kusisitiza ujumbe wa mtunzi.

Katika shairi la 'Ina Nini?' (uk.71) kwa mfano, mbinu hii imetumiwa katika shairi zima yaani kutoka ubeti wa kwanza hadi ubeti wa mwisho. Mtunzi anakamilisha kila mshororo wake kwa swali la balagha. Anatumia maswali haya kusisitiza kuchochea kinachofanya watu kung'ang'ania uongozi. Pia, anatumia maswali haya kuzindua jamii kuhusu tamaa ya watu kutaka kuwa viongozi. Vile vile ametumia maswali haya kuzua taharuki kwa hadhira kudadisi zaidi kinachowafanya watu kung'ang'ania uongozi. Kwa kujiuliza maswali yafuatayo, mshairi anashangaa sababu za watu kutoka matabaka mbali mbali kung'ang'ana ili kuingia siasa:

'Kwa nini, mwalimu darasani, ache kazi ya thamani, akachupia, kwa papara, gari la siasani?

Ni nini, daktari wodini, agure spitalini, akarukia, kwa haraka, gari la siasani?' (ubeti wa 3).

Katika shairi la 'Msalaba' (uk.2), mwandishi amefaulu kutumia mbinu hii kuchochea hisia za wazalendo kukumbuka jinsi walivyosherehekea uhuru kama inavyodhihirika kupitia ubeti wa kwanza ufuatao:

Mama na baba mnakumbuka?
Chereko na cheko mnakumbuka?
Furaha na raha mnaikumbuka?

Shairi la 'Ijumaa' (uk.56) lina matumizi ya mbinu hii katika ubeti wa tatu na ubeti wa tano. Mshairi anajiuliza swali baada ya kukumbuka madhara yaliyosababishwa na ugaidi. Magaidi walikata kata miili ya watu vipande vipande na damu kumwagika na kutapakaa kote.

Je, hii ndiyo njia ya kujiunga na kilinge cha ugaidi wa kimataifa? (kifungu cha tatu uk.56).

Baada ya watu wengi kuiaga dunia na wengine kujeruhiwa kutokana na ugaidi, ilitarajiwa kwamba angalau Hazina ya Maafa ingewaauni waathiriwa. Walichokifanya wanasiasa hao, ni kutoa rambirambi zilizokuwa za kiada na maombolezo. Badala ya kutuma msaada ambao ulihitajika kwa familia za waathiriwa, walianza na kujishughulisha na kuteua kamati nyingine ya Hazina ya Maafa. Mshairi anashangaa kilichofanyika kwa hazina zilizokuwepo. Anauliza swali lifuatalo kuashiria ufisadi wa pesa za umma: 'Hazina ilikwenda wapi?' (uk.57).

### 4.1.6 Urudiaji.

Urudiaji ni hali ya kulisema jambo mara kadha ili kuteka nadhari ya msomaji. Msomaji anapolikumbuka jambo fulani, basi mtunzi huwa ametimiza azimio la kusisitiza na kuliweka

wazi jambo fulani. Mtunzi wa kazi za fasihi hutumia urudiaji ili kuviunga vipengele muhimu vya msuko na kuleta ruwaza fulani. Urudiaji pia hujulikana kama takriri na una umuhimu ufuatao: Hutumiwa kusisitiza ujumbe wa mwandishi ambao anajaribu kuupitisha kwa hadhira. Vile vile, urudiaji huchimuza au kuonyesha toni ya ushairi. Pia, urudiaji hutumiwa kuibua lengo kuu la mwandishi. Maudhui mbalimbali vile vile huibuliwa kutokana na urudiaji. Uradidi bora ni ule utumiao visawe, miundo tofauti ya mnyambuliko ili kuleta athari nzuri ya kiumbuji. Aina mbalimbali za urudiaji zimejitokeza katika diwani *Kaza Macho.*

#### 4.1.6.1 Urudiaji wa Neno

Urudiaji wa neno au maneno ni ule ambapo neno au vifungu vya maneno hurudiwarudiwa. Katika shairi la 'Ina Nini' (uk.71), mtunzi ameradidi neno 'kitini' mwishoni mwa kila mshororo wa ubeti wa kwanza. Anaradidi neno 'bungeni' katika ubeti wa 2, 4, 6, 8 na neno 'siasani' Katika ubeti wa 3,5, na 7. Katika shairi la 'Msalaba' (uk.2), neno 'kumbuka' na 'hongera' limerudiwa rudiwa. Katika shairi la 'Meli, Nini Kiliipata?' (uk.8), neno 'meli' limerudiwa. Katika shairi la 'Mwanasiasa' (uk.11), neno 'mwenye' katika ubeti wa pili na wa tano limerudiwa rudiwa. Kuna urudiaji wa neno 'unakumbuka' katika shairi la 'Mkuki kwa Nguruwe' (uk.51).

Katika shairi la 'Uonacho Sicho' (uk.1), kumesheheni matumizi ya urudiaji huu. Neno 'yote' limerudiwa katika ubeti wa tatu mshororo wa kwanza. Katika shairi la 'Chini ya Mgunga' (uk.53), mbinu hii inajitokeza katika ubeti wa mwisho ambapo neno 'mgunga' limerudiwa kusisitiza masuala ya umasikini.

> 'Mgunga ulikuwa kivuli…
>
> Mgunga ulikuwa msitu wa…' (kifungu cha 3).

Katika shairi la 'Nungubandia' (uk.55) kuna urudiaji wa neno 'mwanasiasa' ambapo neno hilo limeradidiwa kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Tamathali hii imetumika kusisitiza ujumbe anaowasilisha mtunzi kumhusu mwanasiasa ambaye si mtu wa kuaminika.

> Mwanasiasa, mwanasayansi katika maabara ya maisha,
>
> Mwanasiasa, anaufungua mkoba huku anajishasha…

Katika shairi la 'Uliambiwa'(uk.126) kuna takriri ya neno 'uliambiwa' kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Katika shairi la Kaza Macho neno 'mwenye' limerudiwa katika ubeti wa pili kusisitiza ujumbe wa mtunzi na vile vile kuchimuza toni ya mwandisi.

'Mwenye maziwa yaliyoinama kwa ukiwa,

Mwenye macho mekundu kwa sababu ya moshi…'

#### 4.1.6.2 Urudiaji wa Sauti (konsonanti na irabu)

Urudiaji wa sauti ambapo sauti mahususi imerudiwarudiwa katika shairi. Kuna urudiaji wa konsonanti /k/ katika shairi la 'Mkuki kwa Nguruwe' uk.51 kifungu cha 2, '…kukuru kakara, kukuru kakara, kukuru kakara.' Mbinu hii imetumika kuchimuza toni ya shairi.

#### 4.1.6.3 Urudiaji wa Mistari

Urudiaji huu unadhihirika wazi katika shairi la 'Mfumo wa Soko Huria' (uk.3), mstari wa 'soko huria' limerudiwa. Katika shairi la 'Ulifanya Nini' (uk.18), mstari 'unaikumbuka siku' unarudiwa kwa lengo la kuchochea hisia za msomaji. Isitoshe, katika 'Kadhia ya Jana' (uk.21) mstari 'nalikumbuka sana,' umerudiwa rudiwa. Urudiaji huu umetumika katika shairi kusisitiza ujumbe anaowasilisha mtunzi.

#### 4.1.6.4 Epifora

Huu ni urudiaji wa neno au fungu la maneno kwenye sehemu ya mwisho ya mstari. Kwa mfano, katika shairi la 'Ina Nini' (uk.71), maneno mbalimbali yamerudiwa mwishoni mwa mishororo tofauti tofauti ya shairi kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao;

Ubeti wa 1…awe kitini,

Ubeti wa 2…waingie bungeni,

Ubeti wa 3…gari la siasani n.k.

Kupitia urudiaji huu, mwandishi anasisitiza tabia ya watu kutaka kuchukua hatamu za uongozi.

#### 4.1.6.5 Anadiplomasia

Huu ni urudiaji ambapo neno au fungu la maneno linatumika mwishoni mwa mstari mmoja hurudiwa katika mwanzo wa mstari mwingine katika shairi. Kwa mfano, katika shairi la 'Zinduka' (uk.31), fungu la maneno linalomalizia mshororo wa mwisho katika kila ubeti linatumika kuanzia mshororo wa kuanzia ubeti unaofuata. Kwa mfano,

Ubeti wa 1 …ukabakia juhali,

Ubeti wa 2 ukabakia juhali…

Ubeti wa 3 …, kubakia kama boza

#### 4.1.6.6 Anafora

Huu ni urudiaji wa neno au fungu la maneno mwanzoni mwa kila mstari wa ubeti wa shairi. Urudiaji huu vile vile hutumiwa ili kuleta msisitizo wa ujumbe unaokusudiwa. Katika shairi la 'Jana na Leo' (uk.26) neno 'naikumbuka' limerudiwa mwanzoni mwa kila mshororo wa kwanza wa kila ubeti. Vile vile neno jana, hofu, sheria na suti yameanzia mishororo mingine yote kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa tano mtawalia. Katika shairi la 'Nungubandia' (uk.55), neno mwanasiasa linatumika mwanzoni mwa mishororo minne ya kwanza katika kila ubeti.

### 4.1.7 Usambamba

#### 4.1.7.1 Usambamba wa Kitanakuzi

Unahusu mawazo mawili yanayokinzana au yaliyo na maana kinyume. Hii ni mbinu ambapo katika kifungu kimoja cha sentensi, neno moja huwa ni kinyume cha neno lingine. Kwa mfano, baada ya 'huzuni' ni 'furaha'. Mbinu hii hutumika kuonyesha hali mbalimbali za mhusika fulani katika ushairi. Msingi wa usambamba huu ni kauli kinzani ambapo wazo linaloelezwa katika mstari wa kwanza linapingana na lile linalojitokeza katika mstari wa pili. Katika shairi la 'Kibinimethali' (uk.16), mwandishi ametumia usambamba wa kitanakuzi katika ubeti wa kwanza mshororo wa tano anaposema '…imekuwa hatia uwongo kuhalalisha.' Katika ubeti wa tatu vile vile anasema, 'wizi umegeuka halali.'

Kwenye shairi la 'Kikao cha Wanasiasa' (uk.89), mwandishi ametumia hii mbinu katika ubeti wa mwisho anaposema kuwa 'jema' na 'jimbi' yaani zuri na baya kurejelea wanasiasa ambao wanaimba nyimbo za kongole na wamefilisisha nchi yao kutokana na uporaji.

#### 4.1.7.2 Usambamba wa Kifahiwa

Katika usambamba wa kifahiwa, neno fulani huwasilishwa kwa kutumia visawe vyake kwa lengo la kusisitiza ujumbe. Shairi la 'Ndege wako Mashakani' (uk.45) usambamba huu unajitokeza kama ifuatavyo; ndege=kunguru, kipungu, mbuni, mboze na njiwa. Katika shairi la 'Mkuki kwa Nguruwe…'(uk.51) neno mkoloni=mgeni kumrejelea mbeberu aliyetawala mataifa ya Afrika kimabavu.

### 4.1.8 Uhuishi

Hii ni mbinu ambayo vitu visivyo na uwezo wa kuhisi au uhai hupewa sifa za kibinadamu. Binadamu ana upekee wa sifa anuai mfano kucheka, kulia, kutembea, kutabasamu, kulia na kadhalika. Wakati mwingine mwandishi huamua kuvipa vitu visivyo na uhai uhai ili kuiboresha kazi yake ya kisanaa na kuifanya iweze kuvutia. Mfano, mawe hayo yalitabasamu ajabu! Hapa, mawe yamepewa sifa ya kutabasamu ambayo ni ya kibinadamu. Katika shairi la Kaza Macho ubeti wa nne, kuna matumizi ya uhuishi ambapo mwandishi amelipa jumba sifa ya kibinadamu ya kuonja na kutabasamu.

> Penye bahari ya jumba lililopanda juu,
> Linalolionja jua la macheo kabla ya waja,
> Linalorishai nemsi na bashasha za kutajika.

Uhaishaji kama mbinu ya kisanaa, imetumika kuibua picha halisia hasa ya masuala ambayo yanaangaziwa katika ushairi. Kupitia mbinu hii, maudhui vile vile yamekuzwa kwa kina.

### 4.1.9 Chuku

Hii ni mbinu ambapo mwandishi hukuza kitu, hali au dhana fulani kupita kiasi. Katika shairi la ‘Ijumaa’ (uk.56), mbinu hii imejitokeza. Maelezo jinsi ambavyo nyumba zilivyoporomoshwa na kwingine mapaa kuharibiwa ni chuku kama inavyodhihirika kupitia mstari huu; ‘Vigae vilivyopeperushwa peperu na kuyavua majengo kofia kuacha wazi para za miaka.’Mshairi anaonyesha jinsi ambavyo magaidi waliharibu majengo kupitia milipuko ya maguruneti na mabomu. Tamathali hii imetumika kuonyesha hasara iliyosababishwa na ukatili wa magaidi kwa taifa na kwa wananchi wasiokuwa na hatia.

Katika shairi la ‘Kaza Macho’ (uk.17 kifungu cha 4), matumizi ya chuku yanajitokeza. Mshairi anatilia chumvi anapoelezea nyumba za kifahari za matajiri au viongozi kwamba ni kubwa sana kiasi cha kulinganishwa na bahari jambo ambalo si kweli. Mwandishi anasema kuwa ‘bahari ya jumba lililopanda juu na ambalo linaonja jua la mapambazuko kabla ya binadamu wenyewe kufanya hivyo.’ Mbinu hii imetumika kusisitiza ukubwa wa majumba au makasri ya waheshimiwa na kwamba wao huishi maisha ya kifahari huku wananchi wakitaabika katika vibanda vyao.

Akisimulia masaibu waliyoyapitia mikononi mwa mkoloni katika shairi la 'Mkuki kwa Nguruwe' (uk.51), mshairi anatilia maelezo yake chumvi anaposema kwamba mwafrika aliteswa kwa kutozwa kodi ya kuishi, akatokwa na hata jasho la damu' (kifungu cha 1).

### 4.1.10 Kinaya

Mbinu hii hujitokeza pale ambapo mwandishi huhitaji kuleta dhana ya kinyume na matarajio yaani matokeo huwa kinyume pasi kutarajiwa. Katika shairi la 'Mwanasiasa' (uk.11) ni kinaya kuwa mwanasiasa alipofika huko kileleni alipopanda, aliwagota vichwa waliomshikilia ngazi ile (kifungu cha 3 uk.11). Badala ya mwanasiasa huyo kuwasaidia wananchi waliompa nguvu za kutawala aliwageuka na kutumia mamlaka hayo kuwakandamiza.

Mwandishi pia, ametumia mbinu hii ya kinaya katika shairi la 'Kaza Macho' (uk.17). Ni kinaya kuwa ajuza na shaibu walioshiriki katika harakati za kuikomboa nchi wanakosa mavazi, wanaishi katika mabanda na wanakosa chakula ilhali kuna wengine ambao kamwe hawakushiriki katika harakati hizo lakini wanaishi katika majumba ya kifahari na hata wanahesabu pesa kwa mashine ndogo.

Katika shairi la 'Mwanga' (uk.24), ni kinaya kuwa maajuza wanashangilia na kusifia sera mpya hadi kukaukwa na koo ilhali matumbo yao yanawaguguna kwa kukosa chakula huku vigogo matumbo yao yamejaa kabisa.

> …Matumbo yanawaguguna kwa kukikosa chakula (kifungu cha 1).
>
> …Yaone matumbo yao yaliyojaa kabisa (kifungu cha 3).

### 4.1.11 Sitiari/Istiari

Mbinu hii hulinganisha vitu viwili moja kwa moja kwa kuwa vitu hivyo vina sifa au tabia sawa. Mbinu hii inasaidia kuibua picha halisi ya hali au kitu kinachorejelewa kwenye kazi ya fasihi. Pia, huchimuza toni ya shairi na kuibua maudhui mbalimbali yanayoangaziwa na malenga. Mfano Juma ni chui.  Katika mfano huu, Juma amelinganishwa moja kwa moja na chui hivyo kumaanisha ni mkali.

Katika shairi la 'Mwanasiasa' (uk.11), mbinu hii ya sitiari imetumika kwa wingi. Mwanasiasa amelinganishwa moja kwa moja na kijana. 'Mwanasiasa ni kijana,' kurejelea tabia ya utani aliyonayo huyo mwanasiasa kama ilivyo kwa kijana. Katika kifungu cha pili, mwanasiasa

analinganishwa na mpanda ngazi. ‘Mwanasiasa ni mpanda ngazi,’ kuonyesha kwamba mwanasiasa huyo ana matarajio ya kupata makubwa.

### 4.2.0 Mbinu Nyingine za Lugha

### 4.2.1 Methali

Methali huwa ni kauli fupi fupi ambazo huwa na maana ambayo imefumbwa na inamhitaji anayesoma kufikiria zaidi ili kuweza kung’amua maana iliyokusudiwa. Methali huibua dhamira ya mwandishi katika kazi ya kisanaa. Dhima ya methali huwa ni kuelekeza, kusuta, kuadibu kushauri, kukosoa au kuelimisha. Katika Utenzi wa Ndovu na Mja kwa mfano, kuna matumizi ya methali:

> ‘Mpishe mwenye na nguvu,
> Kwa upole na utuvu,
> Au atakuwa mavu,
> Mashavu kushambuliya’ (ubeti wa 54 uk.107).

Methali hii haijajitokeza jinsi ilivyo ‘Mwenye nguvu mpishe.’ Mtunzi aliibadilisha ili kupata urari wa kina ‘vu’ na mizani na hivyo kujitokeza mpishe mwenye na nguvu. Kwa kawaida mtu ambaye ana nguvu kukushinda, inastahili kumwachia njia apite ili ajieendee zake bila kumfungia wala kushindana naye. Methali hii inatumika kutushauri ili tufahamu kikomo na kiwango cha uwezo tulio nao na kukoma kuwa na hulka ya kujitia ujasiri na kushiriki vita na watu ambao wametushinda uwezo. Wamitila ametumia methali hii kuwarejelea wanyonge ambao hawana nguvu za kiuchumi kukoma kushindana na viongozi na badala yake kutafuta mbinu mbadala ya kuwaondoa mamlakani.

Katika shairi la ‘Mkuki kwa Nguruwe’ (uk.51), methali ‘Mkuki kwa nguruwe, kwa binadamu u chungu’ (kifungu cha 3) imetumika. Inaaminika ya kwamba nguruwe anapochomwa mkuki, inaonekana kuwa bora kabisa ila binadamu anapochomwa na huo mkuki, binadamu huyo huona mkuki ule ukiwa na uchungu mwingi. Methali hii inatufunza kwamba tuepuke kuwa na hulka ya kufurahia masaibu ambayo yanawapata wenzetu katika jamii lakini tukahuzunika endapo yamepiga hodi kwetu. Methali hii imetumika kuwashauri viongozi walio na tabia ya kushangilia madhila ya wanyonge katika jamii kukoma na badala yake wawapende kama walivyojipenda. Pia, imetumika kumhamasisha mwafrika dhidi ya kumtesa mwafrika mwenzake na kusuta suala la ukoloni mamboleo.

### 4.2.2 Nahau

Ni kauli fupi fupi ambazo hutumika kutoa maana maalumu ambayo haitokani na ile maana ya kawaida ya maneno yenyewe. Muundo wa nahau huonyeshwa kwa matumizi ya vitenzi na nomino. Kwa mfano, ‘chungulia kaburi’ ambayo ina maana ya kukaribia kupoteza uhai. Inapotumika katika kazi ya kisanaa, nahau hukoleza lugha na kuifanya iwe ya mvuto na mnato.

Kwa mfano, katika shairi la ‘Mkuki kwa Nguruwe’ (uk.51) mshororo wa sita ubeti wa pili, kuna matumizi ya nahau mwandishi anaposema kuwa ‘hatimaye akaubwaga ukoloni chini’ kuashiria mwisho wa utawala wa mkoloni. Katika shairi la ‘Mlevi wa Historia’ (uk.12), nahau zifuatazo zinadhihirika:

Baada ya kupata cheo, viongozi, ‘walilewa chakari na vichwa vyao vikavimba…’ (kifungu cha 1, uk.12). Nahau vimba kichwa inamaanisha kuingiwa na ujeuri au kiburi. Wanasiasa au watawala walipoyapata mamlaka, walijawa na kiburi na hivyo kuanza kuwanyanyasa watawaliwa. Nahau lewa chakari inaamanisha kulewa sana baada ya mtu kunywa pombe. Nahau hii imetumika kuwarejelea viongozi wanaolewa kupitia mamlaka wanayopata na kuwasahau wananchi wakiteseka kwa dhiki.

Kwenye shairi la ‘Uhuru’ (uk.15). Mshairi anaeleza kwamba dini imekuwa hifadhi na ‘Kimbilio la wapiga nchi kabari’ (kifungu cha 4 uk.15). Nahau piga kabari inamaanisha kukaba mtu shingoni kwa kutumia kipingiti cha mkono. Nahau hii imetumika kuashiria jinsi ambavyo watu walio na uwezo mkubwa wa kiuchumi wameipora nchi na kukimbilia maabadini ili kuficha mawindo yao. Nahau hii imetumiwa kukuza maudhui yanayorejelewa na mwandishi katika kazi yake ya sanaa.

### 4.2.3 Taswira

Hii ni mbinu ambapo mtunzi hutoa maelezo ambayo yanaibua picha kamili mawazoni mwa msomaji. Taswira hutumiwa kujenga picha halisi ya jambo linalorejelewa hivyo kukuza dhamira ya mtunzi. Kuna aina mbali mbali za taswira kama ifuatavyo: Taswira mnuso au harufu ambapo harufu fulani hurejelewa au hufafanuliwa. Taswira mguso ambayo huhusisha ukaribiaji wa viumbe au watu. Taswira usikivu ambapo sauti au, mlio fulani hudokezwa k.v. milio ya ndege.

Taswira uoni ambapo maelezo kuhusu jambo au hali fulani hutolewa na hivyo kujenga picha kwenye akili ya msomaji. Mwisho, kuna taswira mwendo ambapo hali au maudhui fulani hukuzwa kikamilifu kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Mbinu hii inadhihirika katika diwani ifuatavyo:

Maelezo kumhusu kijana ambaye alitumwa mafugani kuwapeleka mifugo yao malishoni na baadaye kuanza kulalamika kuhusu mbwa mwitu asiyeonekana yanajenga picha akilini mwa msomaji. Maelezo jinsi ambavyo kijana huyo alipiga ukwenzi kuitisha msaada kutoka kwa marafiki ni taswira sikizi kifungu cha 1 (uk.11) shairi la 'Mwanasiasa.'

Katika shairi la 'Chini ya Mgunga' (uk.53) kuna taswira ambayo inajitokeza ambapo mwandishi anasimulia walivyokuwa wameketi na kuimba kwa sauti herufi zote kuanzia A mpaka Z. Taswira hii inajenga picha ya umasikini katika taasisi za elimu.

> 'Tulikoketi na kuimba kwa,
> Sauti herufi zote…kuanzia A mpaka Z,
> Tulikofunzwa jinsi ya kuandika…' (kifungu cha 1 uk.53).

Katika shairi la 'Ijumaa' (uk.56), kuna matumizi ya taswira ambayo inaonyesha ukatili uliosababisha mauaji na uharibifu wa mali katika ubeti wa pili.

> 'Vigae vilivyopeperushwa peperu na
> Kuyavua majengo kofia kuacha wazi para za miaka.
> Tetemeko kuu lililotingisha na kutikisa kila kitu…'(uk.56)

Katika shairi la 'Kaza Macho' (uk.17), mwandishi amefanikiwa kutumia mbinu hii katika beti zote. Kwa mfano, katika ubeti wa tatu tunapata picha kamili ya shaibu anayesongwa na umasikini tunapoambiwa;

> 'Mkazie macho na yule shaibu;
> Anayekiinamisha kichwa akihesabu vyanda,
> Aliyepinda miguu kama nguzo za banda kuu,
> Anayetokwa na nyute pande mbili za kinywa,
> Aliyechongwa mwili na patasi za maisha…' (kifungu cha 3).

### 4.2.4 Kisengere Nyuma

Hii ni mbinu ambapo mwandishi hujaribu kuyarejelea matukio ya hapo awali au yaliyopita. Katika shairi la ‘Uonacho Sicho’ (uk.1), matukio ya kihistoria kuhusu dhuluma walizotendewa wenyeji na wakoloni yameelezwa kupitia mbinu hii. Wenyeji hao walitumikishwa bila huruma lakini baadaye wakapambana na mkoloni na hatimaye kujikomboa.

Katika shairi la ‘Chini ya Mgunga’ (uk.53), kuna matumizi ya mbinu hii. Msimulizi anakumbuka wakiwa watoto jinsi walivyoketi chini ya mgunga mnene ambako walisomea kwa kuimba herufi za alifabeti. Hapo ndipo walipofunzwa namna ya kuandika kwenye mchanga wakitumia vidole gumba (kifungu cha 1).

**4.2.5 Mdokezo**

Hii ni mbinu ambapo mwandishi hakamilishi usemi wake na huacha msomaji kujikamilishia. Mbinu hii hudokezwa kwa kuwepo kwa alama za dukuduku.

Katika shairi la ‘Mwanasiasa’ (uk.11), tunaipata mbinu hii katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa pili na ubeti wa nne.

> ‘Akawagota vichwa ngazi waliomshikia…’ (ubeti wa pili).
>
> ‘Lakini mwendo wake ni wa haraka…’ (ubeti wa nne).

Katika shairi la ‘Chini ya Mgunga’ (uk.53) kuna matumizi ya mdokezo katika kifungu cha kwanza mstari wa tano na tisa.

> *Sauti herufi zote…kuanzia A mpaka Z* (msitari wa tano) kurejelea herufi za alifabeti katika elimu.
>
> *Tulikoandika kwa madole gumba ya viguu vyetu vya kitoto...* (msitari wa tisa) kwa sababu ya uhaba au ukosefu. wa vifaa vya masomo

Katika shairi la ‘Nungubandia’ (uk.55), mbinu hii imetumika katika beti zote mbili.

> ‘Raia naye…
>
> Ni nungubandia aliyewekwa mezani…’ (uk.55).

Katika shairi la ‘Ijumaa’ (uk.56), hii mbinu imetumika pia katika kifungu cha pili, tano na sita.

> *Ambao walikuwa BADO hawajaanza kuishi…* (kifungu cha pili) labda kurejelea Maisha.

*Kisha baadaye…* (kifungu cha tano).

*Mbali huko nilisikia cheko la fisi…* (kifungu cha sita) likichekelea masikini.

Katika shairi la 'Kichekesho cha Historia' (uk.74), kifungu cha nane na tisa kuna matumizi ya mdokezo.

*'Wenye msisimko…'* (kifungu cha 8 uk.76) labda mkali.

*'Na sauti ile ile…' (*kifungu cha 9 uk.76) ya utani na ulaghai kutoka kwa viongozi.

Katika shairi la Kikao cha Wanasiasa (uk.89), kuna matumizi ya mdokezo katika ubeti wa mwisho.

*'Kuichuna ngozi nchi yao…'* (kifungu cha 3 msitari wa mwisho) ili kuifilisisha.

Mbinu hii imetumiwa na mwandishi ili kuepuka maneno yenye ukali au kukuza tasifida. Mwandishi anatarajia kuwa maneno hayo yaliyoachwa yanaeleweka vyema na msomaji au anayatambua.

### 4.18 Hitimisho

Sura ya nne tumejadili mbinu za kisanaa ambazo K.W. Wamitila ametumia kuwasilisha maudhui ya kisiasa katika diwani *Kaza Macho.* Miongoni mwa mbinu hizo ni pamoja na tamathali za usemi: jazanda, tashbihi, tabaini, tanakali za sauti, maswali ya balagha, urudiaji, usambamba, uhuishi, chuku, kinaya na sitiari. Mbinu nyingine za kisanaa ni: Methali, nahau, taswira, kisengera nyuma na mdokezo. Sura inayofuata, tumeshughulikia matokeo yanayotokana na utafiti wetu. Pia, tumeangazia mapendekezo yetu kwa watafiti wa baadaye.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Kwenye sura hii ya tano, tumeangazia muhtasari wa sura zote, hitimisho na hatimaye kutoa mapendekezo kwa wasomi wa baadaye ambao wananuia kutafiti maudhui ya kisiasa. Tumewasilisha matokeo ya utafiti wetu kwa njia ya maelezo katika sehemu pia. Kwa minajili ya kufanikisha haya, tutatathmini endapo madhumuni ya utafiti huu yameafikiwa kwa kujikita kwenye maswali yetu ya utafiti.

## 5.1 Muhtasari

Tumehakiki maudhui ya siasa na athari zake katika jamii. Tumerejelea diwani, *Kaza Macho.* Kwenye sura ya kwanza, vipengele vifuatavyo vimeshughulikiwa: Tumefafanua tatizo la utafiti wetu na malengo yake. Tumetambua mchango wa wasomi wengine ambao wameandika kuhusu mada hii kwa kurejelea kazi zao. Tumeorodhesha maswali ya utafiti ambayo yamejibiwa katika sura hii ya tano. Kando na kuonyesha mipaka ya utafiti wetu, tumefafanua mbinu za utafiti ambazo zimetumika kukusanya na kuwasilisha data. Nadharia na mihimili yake imefafanuliwa pia.

Katika sura ya pili, dhana ya siasa imefasiliwa kama mfumo wa kijamii ambao unahusu matumizi ya sheria katika kufanya maamuzi ya kiutawala katika asasi mbalimbali za kijamii. Maudhui ya kisiasa yamechanganuliwa ambapo diwani, *Kaza Macho* imerejelewa. Nayo sura ya tatu, tumeshughulikia athari ambazo zinasababishwa na siasa kwa jamii. Baadhi ya athari hizo ni: umaskini, vita na tanzia, tamaa, unyanyasaji na kung’atuliwa kwa viongozi mamlakani.

Kilele cha kazi hii ni katika sura ya nne ambayo imeshughulikia mbinu za kisanaa ambazo mwandishi, K. W. Wamitila ametumia kama nyenzo ya kuwasilisha ujumbe wake. Tumedhihirisha kwamba jazanda ni miongoni mwa tamathali za usemi ambazo zimetumiwa kufanikisha uwasilishaji wa maudhui hayo. Tamathali zingine za usemi ni: Tashbihi, Tanakali za sauti. Maswali ya balagha, urudiaji na usambamba. Mbinu nyingine za lugha ambazo zimefanikisha uwasilishaji wa maudhui ni Pamoja na methali, nahau, kisengere nyuma na taswira.

Tuliongozwa na mihimili ifuatayo ya nadharia ya uyakinifu wa kijamii: kwanza, wahusika wameonyeshwa kwa njia ya kiuyakinifu ambapo tumeonyesha kuwa baadhi ya wahusika katika diwani, wamemithilishwa na binadamu wa kawaida. Mpanda Ngazi na Washika Ngazi katika ukurasa wa kumi na tano, ni mfano mzuri wao. Pili, nadharia hii imesawiri matukio ya kihistoria. Mshairi anatujulisha historia ya jinsi ambavyo mkoloni aliwadharau na kuwakandamiza wenyeji kupitia shairi la 'Mkuki kwa Nguruwe' (uk.51). Mwisho, wahusika wake wametekeleza matendo yao kitabaka kama inavyodhihirika katika shairi la 'Mpanda Ngazi na Washika Ngazi' (uk.15) na 'Utenzi wa Ndovu na Mja' (uk.104).

Utafiti huu ulinuia kutekeleza malengo matatu yafuatayo: kuchanganua namna maudhui ya kisiasa yanavyojitokeza katika *Kaza Macho.* Matokeo ya utafiti wetu yalidhihirisha kuwa maudhui yafuatayo yanajitokeza kwa kiasi kikubwa: uongozi wa kiimla, ukoloni na ukoloni mamboleo, ufisadi, usaliti na ukiukaji wa sheria.

Madhumuni ya pili yalikuwa kubainisha athari za siasa kwa jamii. Matokeo yalibainisha kuwa siasa imeibua athari hasi kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na athari chanya. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na umaskini, tamaa na unyanyasaji, utabaka, vita na tanzia.

Madhumuni ya tatu yalihusu kuchanganua mbinu za kisanaa ambazo zilitumiwa kuendeleza maudhui ya kisiasa katika diwani. Uchunguzi wetu ulibainisha kuwa jazanda, kinaya, tashbihi, maswali ya balagha zimetumika kufanikisha ujumbe. Methali, sitiari, mbinu rejeshi, kinaya, usambamba wa kitanakuzi, usambamba wa kifahiwa na takriri zimefanikisha uwasilishaji wa maudhui haya vile vile.

Maswali yafuatayo matatu yaliweza kuongoza utafiti huu: Ni maswala gani ya kisiasa yanayojitokeza katika *Kaza Macho.* Utafiti wetu ulibainisha kuwa viongozi wametumia siasa kujitafutia umaarufu na kujilimbikizia mali. Viongozi hao wamewasaliti wananchi waliowapigia kura kwa kushiriki katika matendo ya ufisadi. Uongozi wa kiimla unadhihirika wazi katika mataifa haya ambayo hayana uwezo mkubwa wa kiuchumi. Ukoloni mamboleo ndio mtindo wa kiutawala ambao unakumbatiwa na hao viongozi. Visa vya ukiukaji wa sheria na haki za kibinadamu vile vile vimeshuhudiwa.

Swali la pili lilikuwa: Maudhui ya siasa yanaibua athari zipi? Tulibainisha kuwa athari hasi ambazo zinatokana na siasa ni nyingi. Viongozi waafrika walitarajiwa kuboresha maisha ya wananchi wenzao baada ya mbeberu kuondoka. Badala ya kuwasaidia na kuwaokoa kutoka lindi

la ukiwa na ukata, viongozi hao waliwasukumia masaibu zaidi. Waligeuza uzalendo ukawa uhaini na wema ukawa uovu kama inavyodhihirika katika shairi la 'Kadhia ya Jana' (uk.21). Sera iliyoko haijamsaidia mwananchi wa kawaida kutatua matatizo ambayo yanamwandama kila siku. Badala yake, sera hiyo imekuwa ngome ya wanasiasa ambayo imetumika kupora rasilimali za umma na hatimaye kuwakinga ili kukwepa mkono mrefu wa sheria kama inavyojitokeza katika shairi la 'Uhuru' (uk.15).

Swali la tatu lilikuwa: Wamitila (2014) ametumia mbinu gani za kisanaa kuibua masuala ya kisiasa katika diwani? Uchunguzi wetu ulibainisha kwamba jazanda imetumika kwa kiasi kikubwa kuwasilisha maudhui hayo. Mbinu zingine ambazo zimetumika ni methali, tashbihi, kinaya, takriri, taswira, maswali ya balagha, mbinu rejeshi miongoni mwa zingine. Mbinu hizi zilimsaidia mtunzi kueleza yaliyokuwa moyoni bila hofu.

### 5.2 Hitimisho

Katika tasnifu hii, tumeangazia maudhui ya siasa na athari zake katika jamii ambako tumerejelea diwani ya *Kaza Macho.* Nadharia ya uyakinifu wa kijamii imetufaa sana. Utafiti wetu umekuwa wa kimaktaba ambako tumekusanya data kwa kusoma diwani yenyewe na kisha kuichanganua na kutathmini kwa kutumia njia ya uchambuzi wa kimaelezo. Matokeo yake yamewasilishwa kupitia njia ya maelezo na ufafanuzi.

Matokeo ya utafiti wetu yamebainisha kuwa viongozi wametumia siasa kujitafutia umaarufu na kujilimbikizia mali. Viongozi hao wamewasaliti wananchi waliowapigia kura kwa kushiriki katika matendo ya ufisadi. Visa vya ukiukaji wa sheria na haki za kibinadamu vimeshuhudiwa. Viongozi waligeuza uzalendo ukawa uhaini na wema ukawa uovu kama inavyodhihirika katika shairi la 'Kadhia ya Jana' (uk.21). Sera iliyoko haijamsaidia mwananchi wa kawaida kutatua matatizo ambayo yanamwandama kila siku. Badala yake, sera hiyo imekuwa ngome ya wanasiasa ambayo imetumika kupora rasilimali za umma na hatimaye kuwakinga ili kukwepa mkono mrefu wa sheria kama inavyodhihirika katika shairi la 'Uhuru' (uk.15).

Tumebaini kuwa maudhui ya kisiasa yamepewa kipao mbele na K.W. Wamitila katika diwani hii *Kaza Macho*. Baadhi ya maudhui ni uongozi wa kiimla, ukiukaji wa haki za kibinadamu, usaliti, ufisadi, ukoloni na ukoloni mamboleo. Uongozi huu wa kiimla kwa mfano, umechangia kuongezeka kwa umaskini, kudorora kwa viwango vya elimu na hatimaye kuzua mapigano na

mauaji miongoni mwa jamii hasa wakati wa uchaguzi. Diwani hii imedhihirisha kuwa siasa huwa asasi muhimu kwa jamii na hutumika kuleta sio tu migongano ya kijamii bali hata mshikamano wa wanajamii.

### 5.3 Mapendekezo

Tunapendekeza kuwa watafiti wa baadaye wachunguze maudhui hayo ya kisiasa kwa kurejelea tanzu nyingine k.v. hadithi fupi. Tunapendekeza vile vile kuwa, uchunguzi zaidi wa diwani hii *Kaza Macho* ufanywe kuhusu masuala ya tamaa, ukatili kwa wanyonge, ukiukaji wa sheria na mauaji. Nadharia nyingine ya umaksi au uhalisia inaweza kutumika. Tunapendekeza pia, uchunguzi ufanywe kuhusu jinsi ambavyo bara la Afrika linavyoweza kujikomboa na kuepuka matatizo ambayo yanahusiana na siasa k.v. utabaka na umaskini. Uchunguzi unaweza kufanyika katika utanzu wa ushairi au tanzu zingine za fasihi kama vile hadithi fupi au tamthilia.

## Marejeleo


Adero, M. C. (2005). *Uwezo wa Lugha katika Matini ya Siasa Nchini Kenya.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Amata, K., & King'ei, K. (2001). *Taaluma ya Ushairi.* Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

BAKITA. (2015). *Kamusi kuu ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Bibiana, M. A. (2014). *Kuchunguza Masuala ya Kisiasa katika Riwaya za Shaaban Robert: Mfano wa Kusadikika na Kufikirika.* Dar es Salaam: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).

Brecht, B., & Patrick, D. (1973). *Intellectuals and Class Struggle.* Berlin: New Germany Critique Press.

Chacha, N. C. (1980). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Daily Nation. (23th November, 2020). Africa Suffers when Presidents think they are too big to Retire. In J. Muthama. Nairobi: Nation Media Group Press.

Fanon, F. (1963). *The Wretched of The Earth.* New York: Grove Press Incl.

Gachukia, D. (2005). Government by Tribe or Government by Political Parties? *In Wanjohi, G. J. & Wanjohi, G.W. (Eds). Social & Religious Concerns of East Africa*, uk. 101-107.

Godbole, P. G. (2013). *Mergers and Restructuring.* New York: Vikas Publishing House Pvt. Ltd.

Gorky, M. (1973). *The Lower Division.* London: The Viking Press.

Haugerud, A., & Njogu, S. K. (1991). *State Voices in the Countryside Politics and the Kenyan Baraza, African Studies Center.* Boston: Boston University Press.

Kibwana, K. (1996). Mustakabali wa Mabadiliko ya Katiba Nchini Kenya. In K. Kibwana, G. K. Kimondo, & J. T. Gathii, *Mwananchi na Katiba* (uk. 44-46). Nairobi: Claripress.

Kilonzo , P. K. (2015). *Ujitambuzi Na Utambulisho wa kijinsia katika Riwaya ya Maisha Kitendawili.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kilonzo, P. K., & Masaku, G. M. (2018). *Mwongozo wa Riwaya ya Chozi la Heri.* Nairobi-Kenya: Globalink Publishers Ltd.

Kimeu , N. A. (2016). *Maudhui ya Ukombozi katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kiptum, T. J. (2017). *Uyakinifu wa Maudhui katika Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kothari, R. C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Lucaks, G. (1963). *The Meaning of Contemporary Realism.* London: Merlin Press.

M'ngaruthi, K. T. (2015). *Usawiri wa Mwanasiasa wa Afrika katika Ushairi wa Kiswahili.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Chuka (Haijachapishwa).

Mohamed, K. Y. (2013). *Masuala ya Kisiasa katika Ushairi wa Kandoro.* Dar es Salaam: Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).

Muriithi , J. K. (2013). *Athari za Kidini katika Utenzi wa Rasilghuli.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Njogu , S. K. (1987). *Maudhui ya Mapinduzi katika Riwaya za Viziwani Zanzibar.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Nyong'o, A. (2001). *Governance and Poverty in Africa. The African Academy of Sciences.* Nairobi: Development Bank Press.

Omary, M. (2011). *Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa Karibu Ndani (1988) na Dhifa (2008).* Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Dar es Salaaam (Haijachapishwa).

Osango, S. D. (2015). *Ukombozi wa Kisiasa na Kiuchumi Katika Mkamandume.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Owallah, K. O. (2013). *Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Nabii Isa.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Rono, P. (2013). *Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa Kidagaa Kimemwozea.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Senkoro, F. (1987). *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaam: Press and Publicity centre.

The Standard News Paper. (11th November, 2020). *Seven CSs and 11 Governors Among Big Fish in Haji's Net. In Kwamboka, E.* Nairobi: Standard Media Press.

The Standard News Paper. (15th December, 2020). *Families Marry off Daughters to Easy Finances Amid Covid-19. In AP.* Nairobi: Standard Media Press.

Thuranira, S. I. (2017). *Maudhui ya Ukoloni Mamboleo katika Tamthilia Teule za Kiswahili.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford Publishers.

Waliaula, K. A. (2009). *The Incarcerated Self Narratives of Political confinement in Kenya.* Ohio: Unpublished PhD Dissertation, Ohio State University.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (2014). *Kaza Macho.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wamitila, W. K. (2008). *Kanzi ya Fasihi. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.